

## Table of Contents

UTANGULIZI: .....	4
SURA YA KWANZA: Jina na Makao Makuu ya Umoja .....	4
SURA YA PILI .....	4
Fasili: .....	4
SURA YA TATU .....	6
Madhumuni na huduma zitolewazo na Umoja: .....	6
3.1    Umoja wa KANONO umeanzishwa kwa madhumuni yafuatayo:- .....	6
Taratibu za Utoaji wa Huduma .....	8
3.4    Masharti ya Jumla kwa huduma .....	8
3.6    Wanafamilia wanaotambuliwa na kuhudumiwa .....	9
3.6.1    Wafuatao ni wanafamilia wanaostahili kuhudumiwa:- .....	9
SURA YA NNE .....	10
Uanachama kwenye Umoja .....	10
Kujiunga na Umoja .....	11
Haki za Mwanaumoja .....	12
Wajibu wa Mwanaumoja .....	12
Kukoma kwa Uanachama .....	12
SURA YA TANO .....	13
Mwanaumoja Kuadhibiwa .....	13
Utaratibu wa Kumfukuza Mwanaumoja .....	14
Utaratibu wa Kupeleka Mashauri Mbele ya Kamati ya Nidhamu Na Maadili .....	15
Kukata Rufaa .....	15
SURA YA SITA .....	16
Mfuko wa Umoja: .....	16
Vyanzo vya Mapato vya Mfuko Mkuu .....	16
Masharti yatakayotawala malipo na matumizi ya Mfuko Mkuu .....	17
Mfuko wa Kanda .....	19
Mikopo kwenye Umoja .....	19
Kuchelewesha Mkopo .....	19

Kushindwa kulipa Mkopo.....	19
SURA YA SABA:.....	20
Vikao vya Umoja na Majukumu yake.....	20
Mkutano Mkuu .....	20
Njia itakayotumika kuwaalika Wajumbe wa Mkutano Mkuu.....	20
Namna ya kutuma Ujumbe wa Mwaliko .....	21
Majukumu ya Mkutano Mkuu.....	21
Halmashauri.....	21
Vikao vya Halmashauri.....	22
Majukumu ya Halmashauri .....	22
Kamati Kuu.....	23
Vikao vya Kamati Kuu.....	24
Majukumu ya Kamati Kuu .....	24
Kamati za Kikatiba .....	25
Kamati ya Nidhamu na Maadili .....	26
Kamati ya Rufaa .....	26
Kamati ya Fedha na Uchumi.....	27
Kamati ya Huduma za Jamaii.....	27
Kamati Maalum.....	27
Baraza la Wazee na Kamati ya Wazee.....	28
Kamati ya Uchaguzi.....	29
Kanda .....	29
Kuhama Kanda .....	30
Vikao vya Kanda .....	30
Wajibu wa Viongozi wa Kamati Kuu kwenye Vikao vya Kanda.....	31
Majukumu ya Kanda .....	32
SURA YA NANE.....	32
Sifa za Viongozi: .....	32
Kipimo cha Uongozi wa Umoja .....	33
Masharti ya kuwa Kiongozi kwenye Umoja.....	34
SURA YA TISA .....	34
Uchaguzi wa Viongozi .....	34

Viongozi kujiuzulu .....	34
Upatikanaji wa Viongozi: Mchakato kwenye Kanda.....	35
Kukabidhi Majina Kamati ya Wazee .....	35
Kuteua Wagombea wa Uongozi .....	36
Utaratibu wa Kuwachagua Wajumbe wa Kamati za Kikatiba .....	37
Uchaguzi wa Viongozi wa Kanda na Kamati za Kikatiba .....	38
Wasimamizi wa Uchaguzi kwenye Kanda na Kamati za Kikatiba.....	38
Utaratibu wa Uchaguzi kwenye Kanda.....	38
Kuwasimika Viongozi .....	39
Masuala yanayoweza kumfanya Mwanaumoya asichaguliwe kuwa kongosi .....	39
SURA YA KUMI .....	39
Majukumu ya Viongozi.....	39
10    Majukumu ya Viongozi.....	39
10.1    Viongozi wa Umoja katika utekelezaji wa kazi zao za kila siku watakuwa na majukumu yafuatayo:- ..	39
10.1.2    Makamu Mwenyekiti ni Msaidizi wa Mwenyekiti na ambaye atafanya kazi zote za Mwenyekiti kama:-	40
10.1.6    Mweka Hazina Msaidizi ni Msaidizi wa Mweka Hazina ambaye atafanya kazi zote za Mweka Hazina kama hayupo na kazi nyinginezo kwa maelekezo ya Mweka Hazina au mamlaka nyingine. ....	41
10.1.7    Mwenyekiti wa Kamati atakuwa na majukumu yafuatayo:- .....	41
10.1.8    Katibu wa Kamati atakuwa na majukumu yafuatayo:- .....	41
10.1.9    Mweka Hazina wa Kamati atakuwa na majukumu yafuatayo:- .....	41
10.1.10    Mwenyekiti wa Kanda atakuwa na majukumu yafuatayo:- .....	42
10.1.11    Katibu wa Kanda atakuwa na majukumu yafuatayo:- .....	42
10.1.12    Mweka Hazina wa Kanda atakuwa na majukumu yafuatayo:- .....	42
SURA YA KUMI NA MOJA .....	43
Uwajibikaji wa Viongozi .....	43
SURA YA KUMI NA MBILI.....	44
Marekebisho ya Katiba .....	44
SURA YA KUMI NA TATU .....	45

## UTANGULIZI:

Sisi watu wenye asili ya **Wilaya za Karagwe na Kyerwa** tunaishi **Arusha** kwa pamoja, tumeamua kuanzisha umoja wetu ujulikanao kama KANONO GROUP ambao utaongozwa kwa mujibu wa Katiba hii kama nguzo na dira yake. Madhumuni ya Umoja yatakuwa ni yale tu yaliyoorodheshwa kwenye ibara ya tatu ya Katiba hii ambayo yanalenga kusaidiana na kushirikiana katika masuala ya elimu, na kuisaidia jamii nzima ya Watanzania hasa wale waishio katika mazingira magumu pale mfuko wa Umoja utakapokuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Sifa za Mwanaumoja wa KANONO GROUP zitakuwa ni zile zilizoorodheshwa katika ibara ya nne ya Katiba hii. Umoja huu ulioanzishwa mwaka 1996 ulikuwa na Katiba. Kwa hiyo masuala yote yaliyomo katika katiba hii ni maboresho ya katiba zilizotangulia. Hadi sasa umoja una jumla ya familia zinazotambulika kama Wanaumoja 152 na vile vile Umoja unamilki mali. Kwa misingi hiyo Katiba hii inarithi madeni ya kudai na kudaiwa na mali zote za umoja zilizopatikana kipindi chote kabla ya kupitishwa na kutumika kwa Katiba hii.

## SURA YA KWANZA: Jina na Makao Makuu ya Umoja

**1.1 Jina la Umoja ni KANONO GROUP**

**1.2 Makao Makuu ya Umoja: ARUSHA MJINI, S.L.P 1098, ARUSHA.**

## SURA YA PILI

### Fasili:

**2.1 Kwa minajili ya Katiba hii na kwa tafsiri ya Umoja, wanaumoja tunakubaliana kwamba mambo yafuatayo yatakuwa na maana zifuatazo:**

**2.1.1 Umoja:** Maana yake ni “KANONO GROUP”

**2.1.2 Katiba:** Ni sheria mama itakayosimamia uendeshaji wa shughuli za “KANONO GROUP”; ambayo itatumika kusimamia na kuelekeza fikra, mitazamo na maono ya wanaumoja ili kufikia malengo na madhumuni ya uanzishwaji wa Umoja.

**2.1.3 Kanuni:** Miongozo ya jumla inayowezesha utekelezaji bora wa atiba ya Umoja.

**2.1.4 Viongozi wa Umoja:** Ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Katibu Mkuu Msaidizi, Mweka Hazina, Mweka Hazina Msaidizi, Viongozi na wajumbe wa Kamati za Kikatiba; na Viongozi wa Kanda.

**2.1.5 Viongozi wa Kanda:** Mwenyekiti wa Kanda, Katibu wa Kanda na Mweka Hazina wa Kanda

**2.1.6 Viongozi wa Kamati za Kikatiba:** Ni Mwenyekiti wa Kamati, Katibu wa Kamati, Mweka Hazina wa Kamati na wajumbe wa Kamati

**2.1.7 Mwenyekiti:** Kiongozi na msimamizi mkuu wa shughuli zote za Umoja;

**2.1.8 Makamu Mwenyekiti:** Msaidizi wa Mwenyekiti wa Umoja;

**2.1.9 Katibu Mkuu:** Mtendaji na mratibu mkuu wa shughuli za Umoja;

**2.1.10 Katibu Mkuu Msaidizi:** Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja;

**2.1.11 Mweka Hazina:** Msimamizi wa Taratibu za fedha za Umoja; na

- 2.1.12 *Mweka Hazina Msaidizi:*** Msaidizi wa Mweka Hazina wa Umoja
- 2.1.13 *Mwanaumoja:*** ni mwanaume au mwanamke asiye na ndoa au mke na mume walio na ndoa inayotambulika kwa mujibu wa sheria za nchi, ambao kwa pamoja watahesabika kama mwanaumoja mmoja. Hata hivyo, kwa minajili ya kupiga kura kwenye mikutano ya umoja, kila mmoja wao (mke na mme) atakuwa na haki ya kupiga kura kipekee;
- 2.1.14 *Uongozi:*** Ni dhamana ambayo imekabidhiwa kwa baadhi ya Wanaumoja ili waongoze wanaumoja na Umoja kwa ujumla ili kufikia malengo ambayo wanaumoja wamejiwekea. Kama mme au mke, mmojawapo atachaguliwa kuwa kiongozi wa umoja, aliyechaguliwa ndiye kiongozi na siyo mwenzi wake. Ushirika unabakia kwenye uanachama na siyo majukumu aliyokabidhiwa mmoja wao kama kiongozi;
- 2.1.15 *Mwanachama:*** ni Mwanaumoja kwa maana ya tafsiri ya kifungu cha 2.1.13;
- 2.1.16 *Familia:*** Mume, mke na watoto ambao ni wategemezi kwa mujibu wa sheria za nchi. Endapo mume atakuwa na zaidi ya mke mmoja, kila mke wa ziada anaweza kujiunga na umoja kipekee vinginevyo hatatambuliwa kama mwanaumoja;
- 2.1.17 *KANONO DAY:*** Ni sherehe itakayofanyika Jumapili ya mwisho ya mwezi Julai kila mwaka;
- 2.1.18 *Majukumu maalum:*** Ni majukumu ambayo, kwa uamuzi wa viongozi au mkutano Mkuu, yamekabidhiwa kwa mwanaumoja kwa sababu ya muda, nafasi, uwezo au sifa alizonazo ili ayatekeleze kwa niaba ya Umoja;
- 2.1.19 *Vikao na Mikutano ya Umoja:*** Ni vikao na/au mkutano mkuu, mkutano mkuu wa dharura, kikao cha Halmashauri, Kikao cha kamati kuu, Kikao cha kanda na Kikao cha kamati ya Katiba. Kwa maana hii maneno “vikao na mikutano” vitakuwa na maana ya wajumbe wa makundi yaliyotajwa ambao wamekaa pamoja kwa mujibu wa masharti ya katiba hii;
- 2.1.20 *Kamati ya Uchaguzi:*** ni viongozi wa kanda ambao ni wenyeviti wa kanda na makatibu wa kanda zote;
- 2.1.21 *Kamati za Kikatiba:*** Ni Kamati za Umoja zilizoanzishwa kwa mujibu wa Katiba hii;
- 2.1.22 *Kamati za kikatiba za Kudumu:*** Ni Kamati ya Nidhamu na Maadili, Kamati ya Rufaa, Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Huduma za Jamii na Kamati ya Wazee;
- 2.1.23 *Kamati Maalum:*** Ni kamati ambayo imeundwa na aidha mkutano Mkuu au Halmashauri kwa ajili ya kuchunguza jambo maalum na kutoa taarifa kwa mamlaka iliyoionda.
- 2.1.24 *Baraza la wazee:*** Ni baraza la wanaumoja wote waliofikisha umri wa miaka 55 au zaidi;
- 2.1.25 *Kanda:*** Ni kikundi cha wanaumoja wanaoishi kwenye maeneo yanayokaribiana ambacho kimeundwa na Kamati Kuu kwa mujibu wa katiba kwa madhumuni ya kurahisisha uendeshaji wa shughuli za Umoja. Kanda siyo umoja unaojitegemea na haitakuwa na maslahi yake ambayo siyo ya Umoja katika ujumla wake;
- 2.1.26 *Mwanaumoja Hai:*** Ni mwanaumoja/mwanachama ambaye hana malimbikizo ya ada ya miezi mitatu au zaidi au ambaye hajafungiwa huduma kwa mujibu wa katiba;
- 2.1.27 *Ada:*** Ni kiasi cha fedha ambacho kila mwanachama anachangia kwenye mfuko mkuu wa Umoja au mfuko wa Kanda kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Umoja;
- 2.1.28 *Kutunisha:*** Ni kiasi cha fedha ambacho wanaumoja wote wanachangia ili kurudisha kiasi cha fedha kilichopungua kwenye kima cha chini cha mfuko mkuu wa Umoja. Kiasi hiki

kinachangwa iwapo kiasi cha ada ya Umoja na vyanzo vingine vya mapato haviwezi kurudisha kiasi cha fedha kilichopungua kwenye kima cha chini cha mfuko mkuu wa Umoja ndani ya miezi sita;

- 2.1.29 Harambee:** Ni kiasi cha fedha ambacho mwanaumoja anaahidi kuchangia na kuwajibika kulipa ndani ya miezi sita tangu tarehe ya harambee;
- 2.1.30 KANONO SACCOS:** Ni Chama cha Ushirika cha Kuweka na Kukopa cha KANONO ambacho kilianzishwa kwa uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Umoja kwa ajili ya kuinua hali za wanaumoja kiuchumi na kijamii; na
- 2.1.31 Data base:** Ni mfumodata wa kompyuta wa kuingiza na kuhifadhi kumbukumbu za Umoja na Wanaumoja.

## SURA YA TATU

### Madhumuni na huduma zitolewazo na Umoja:

#### 3.1 Umoja wa KANONO umeanzishwa kwa madhumuni yafuatayo:-

- 3.1.1 Kutegemea uwezo wa Umoja kifedha, kutoa misaada ya kielimu kwa watoto waishio katika mazingira magumu;
- 3.1.2 Kutegemea na uwezo wa mfuko kutoa au kuchangia gharama za matibabu kwa wasiojiweza;
- 3.1.3 Kushirikiana na kusaidiana wakati wa shida na raha mbalimbali;
- 3.1.4 Kuhamasisha Wanaumoja ili kwa hiari na rasimali zao kusaidiana wakati wa raha na shida mbalimbali zisizotolewa huduma kwa mujibu wa Katiba;
- 3.1.5 Kufanya shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii kadri ya mahitaji, maamuzi na uwezo wa mfuko wa Umoja;
- 3.1.6 Kudumisha utamaduni na mila za Wilaya za Karagwe na Kyerwa na utamaduni wa Mtanzania kwa ujumla;
- 3.1.7 Kujenga mwenendo na tabia nzuri kwa Wanaumoja bila kuingilia uhuru wa mtu; na
- 3.1.8 Kuendelezana, kushauriana, kufarijiana, kuwasiliana na kutembeleana.
- 3.1.9 Kuhamasisha Wanaumoja kujiunga na KANONO SACCOS ili:-
  - (a) Kujipatia mikopo kwa ajili ya masomo kwa kiasi cha fedha kinachweza kukidhi mahitaji ya kila mmoja;
  - (b) Kujipatia mikopo ya kuendeleza biashara na kujiongezea kipato; na
  - (c) Kujipatia mikopo ya kijamii kama vile ya ujenzi na ununuzi wa vyombo vya usafiri.
- 3.1.20 Kuhamasisha wanaumoja kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wafaidi fao la afya na wanufaike na pension ya uzeeni;
- 3.1.21 kuhamasisha wanaumoja kujiunga na bima nyingine za afya.

## *Huduma zinazotolewa na Umoja*

### **3.2 Umoja utatoa Huduma zifuatazo:**

- 3.2.1 Kutegemeana na uwezo wa kifedha, kumpatia karo ya shule, kwa kiwango cha ada ya shule ya serikali, mtoto wa Mwanaumoja ambaye amepoteza uwezo wa kufanya shughuli za kiuchumi au kufikwa na mauti wakati akiwa ni Mwanaumoja hai. Karo itatolewa kwa idadi ya watoto ifaayo kwa wakati mmoja kulingana na uwezo wa mfuko na maamuzi ya Mkutano Mkuu;
- 3.2.2 Kumpatia mchango wa matibabu kwa mwanaumoja au mtegemezi mgonjwa ambaye amelazwa hospitali kwa siku tatu (3) au zaidi;
- 3.2.3 Huduma ya kulazwa hospitali inaweza kutolewa kwa mwanaumoja au mtegemezi mgonjwa ambaye kwa hali ya ugonjwa wake anaweza kuruhusiwa kutoka hospitali au hata pengine asilazwe kabisa lakini kwa namna alivyougua, ugonjwa utamlazimu kuugulia nyumbani zaidi ya mwezi bila kupona. Itakuwa kinyume cha katiba kutoa huduma hii kwa mgonjwa aliyegua akabakia nyumbani bila kwenda kupata matibabu hospitali;
- 3.2.4 Kumpatia Mwanaumoja anayesafirisha msiba kwenda Kyerwa, Karagwe au sehemu nyingine nje au ndani ya mkoa mitatu kutoka msiba ulipotokea kwa viwango vya fedha vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Umoja;
- 3.2.5 Kumpatia Mwanaumoja hai anayehamia nje ya mkoa wa Arusha na kuamua kukomesha Uanachama wake baada ya kukaa kwenye umoja kwa miaka isiyopungua minne;
- 3.2.6 Kumpatia Mwanaumoja ambaye atapata au mtegemezi wake atapata ubarikio, kipaimara au tukio jingine la kiimani lililokubaliwa na kutambuliwa kwa misingi ya imani ya dini yake. Huduma hii itatolewa kwa tukio moja kwa kila mwanaumoja au mtegemezi wake;
- 3.2.7 Mwanaumoja atakayeolewa au kuoja atalipwa kiasi cha fedha kilichoainishwa kwenye kanuni za umoja;
- 3.2.8 Mwanaumoja atakayefanya harusi ya kuoza binti au kijana kuoja atalipwa kiasi cha fedha kilichoainishwa kwenye kanuni za umoja. Kwa minajili ya ufafanuzi kuoja au kuolewa kwa mtoto wa Mwanaumoja ni kufunga ndoa inayotambuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi;
- 3.2.9 Kumpatia mwanaumoja kiasi cha fedha kitakachoainishwa kwenye Kanuni kwa ajili ya nauli kwa msiba uliotokea sehemu ya mbali ambao kwa sababu za umbali wanaumoja wameshindwa kushiriki. Huduma hii itatolewa kwa wanaumoja wote ambao undugu wao na aliyefariki unatambuliwa na kuhudumiwa kwa mujibu wa katiba;
- 3.2.10 Kuhudhuria na kutoa pole kwa Mwanaumoja aliyehudumiwa kwa mujibu wa kifungu cha 3.2.9 atakaporudi kutoka msibani na kumlipia kila Mwanaumoja, bila kujali kama ni hai, kwa ajili ya vinywaji na chakula wakati wa tukio hilo.
- 3.2.11 Kumpatia mwanaumoja mgonjwa ambaye kutokana na hali yake kiafya ameamua kwenda kuugulia eneo lililoko nje ya Mkoa wa Arusha na kwa hiari yake na mwenzi wake kuamua kusitisha uanachama wake kwa kuandika barua ya kujitoa kwenye Umoja. Huduma hii haitatolewa mpaka:
  - (a) Awe ni Mwanaumoja hai;
  - (b) awe amepoteza matumaini ya kupona;
  - (c) awe amekubaliana na mwenza wake kujiondoa kwenye Umoja; na

(d) iwapo atapona na kurudi atalazimika kujiunga upya.

- 3.2.12 Kwenye msiba au tukio la kutoa pole, kila mwanaumojwa atatoa mkono wa pole usiopungua kiasi cha fedha kitakachoainishwa kwenye Kanuni.
- 3.2.13 Wanaumojwa wanaoishi nje ya Mkoa wa Arusha watawajibika kutoa mkono wa pole;
- 3.2.14 Wanaumojwa wote watatoa mkono wa pole kwa mwanaumojwa anayeishi nje ya Mkoa wa Arusha au ndani lakini kwa sababu ya umbali hawakushiriki msiba.

### **Taratibu za Utoaji wa Huduma**

- 3.3 Umoja utafuata utaratibu ufuatao katika kutoa huduma kwa matukio mbalimbali:
  - 3.3.1 Kiasi cha fedha kitatolewa kwa Kamati ya Huduma za Jamii kuandaa chakula kwa ajili ya mkusanyiko wa msiba au tukio la kutoa pole;
  - 3.3.1 Kiasi cha fedha kitatolewa kwa Kamati ya Huduma za Jamii kwa ajili ya kuandaa chakula, kununua maji na soda; na kukodi viti;
  - 3.3.2 Kiasi cha fedha au vitu vitakavyobaki baada ya kutoa pole au kuhudumia msiba kwa mujibu wa kitakabidhiwa kwa mfiwa;
  - 3.3.3 Kiasi cha fedha kitatolewa kwa Kamati Kuu ili kwa kushirikiana na familia ya mfiwa kulipia gharama za hospitali, kuandaa mwili, kuchonga jeneza na kuchimba kaburi;
  - 3.3.4 kila mwanaumojwa atatoa mkono wa pole usiopungua kiasi cha fedha kitakachoainishwa kwenye Kanuni.
  - 3.3.5 Wanaumojwa wanaoishi nje ya Arusha watawajibika kutoa mkono wa pole; na
  - 3.3.6 Wanaumojwa wote watatoa mkono wa pole kwa mwanaumojwa anayeishi nje ya Mkoa wa Arusha au ndani lakini kwa sababu ya umbali wanaumojwa hawakushiriki msiba.

### **3.4 Masharti ya Jumla kwa huduma**

- 3.4.1 Msiba unaosafirishwa ndani ya mikoa mitatu lazima safari hiyo isiwe chini ya Kilomita miamoja (Km 100) kutoka msiba ulipotokea;
- 3.4.2 Kuvuka mikoa mitatu kuna maana ya kuingia na kutoka kwenye mipaka ya mikoa. Hii haitajumuisha Mkoa ambao safari inaanzia na Mkoa Safari inapoishia;
- 3.4.3 Huduma ni ya kusafirisha msiba siyo ya kusafirisha ndugu, hivyo huduma hii itatolewa bila kujali idadi ya wanaumojwa ambao wameguswa au wanaotegemea kusafiri;

### **Wajibu wa kuthibitisha Uhalali wa Huduma**

- 3.5 Uthibitisho wa Huduma iliyotolewa
  - 3.5.1 Mwanaumojwa yeyote aliyelipwa fedha ya huduma anawajibika kuwasilisha kwa Mweka Hazina vielelezo vifuatavyo:
    - (a) Kivuli cha cheti cha kifo (death certificate) kama huduma iliyotolewa ilihusu kifo;
    - (b) Barua ya Afisa Mtendaji wa Kijiji kama msiba umetokea kwenye mazingira ambayo cheti cha kifo hakiwezi kupatikana;



- (c) Fomu ya kuruhusiwa kutoka hospitali (discharge summary) kama huduma iliyotolewa ilihusu kulazwa hospitali;
- (d) Kivuli cha cheti cha tukio la kiimani kama huduma iliyotolewa ilihusu tukio la namna hiyo;
- (e) Kivuli cha cheti cha ndoa kama huduma iliyotolewa ilihusu kuoza, kuolewa, kuoza au kuoza; na
- (f) Vielelezo vingine kulingana na huduma iliyotolewa au uamuzi wa uongozi;

3.5.2 Mmwanaumwa atakayeshindwa kuwasilisha vielelezo vya huduma ndani ya siku sitini atalazimika kurudisha fedha aliyopewa kama huduma.

### *Wanafamilia wanaotambuliwa*

3.6 Wanafamilia wanaotambuliwa na kuhudumiwa

3.6.1 Wafuatao ni wanafamilia wanaostahili kuhudumiwa:-

- (a) Mme au Mke mmoja;
- (b) Watoto wanne wa kuzaa au kuasili kwa mujibu wa sheria;
- (c) Baba na mama; na
- (d) Baba Mkwe na Mama Mkwe.

3.6.2 Wanafamilia watakaotambuliwa na kuhudumiwa ni sharti:-

- (a) Wawe wamejazwa kwenye fomu ya taarifa za Mwanaumwa;
- (b) Watoto wawe chini ya umri wa miaka 18 au kama mtoto ana umri wa zaidi ya miaka 18 kivuli cha kitambulisho cha shule au chuo kiambatanishwe kwenye fomu ya kuomba huduma;
- (c) Watoto wawe ni wa kuzaa au kuasili kwa mujibu wa sheria za nchi;
- (d) Mtoto aliyefikisha umri wa miaka 18 hatahudumiwa hata kama ni mwanafunzi iwapo ana familia, amedahiliwa chuoni kusoma shahada ya uzamili au uzamivu.

3.6.3 Iwapo mwanaumwa amelewa kwenye familia ambayo baba au mama ni mzazi wa kufikia:-

- (a) Anaweza kumjaza baba au mama mzazi;
- (b) Baba au mama wa kufikia; na
- (c) Kama amemjaza baba au mama wa kufikia hataruhusiwa kumjaza baba au mama mzazi; vivyo hivyo kama amemjaza baba au mama mzazi hataruhusiwa kumjaza baba au mama wa kufikia.

### *Ndoa kwenye Umoja*

3.7 Ndoa

3.7.1 Mke au mume wa Mwanaumwa atatambuliwa iwapo:-

- (a) Wamefunga ndoa kwa mujibu wa imani na masharti ya imani ya dini ya aidha mwanaumwa au mwenza wake;
- (b) Wamefunga ndoa ya kiserikali; na
- (c) Wamefunga ndoa ya Kimila.

3.7.2 Ndoa itachukuliwa kuwa ya kimila iwapo kuna mojawapo ya mambo yafuatayo:-

- (a) Mwanaumoja ameishi na mume/mke kwa zaidi ya miaka miwili mfululizo;
  - (b) Jamii inayowazunguka (Kanda) inawatambua kuwa mume na Mke; na
  - (c) Wamejitambulisha kwa familia ya mwanamke wakapokelewa na kutambuliwa.
- 3.7.3 Umoja utachukulia kwamba hakuna ndoa endapo:-
- (a) wanandoa wametengana kwa talaka ya Mahakama;
  - (b) kuzaa watoto ndicho kigezo pekee kinachounganisha mwanaumoja na mwanaume/mwanamke;
  - (c) ndoa imehitimishwa rasmi kwa taratibu za imani ya dini husika kama vile kutoa talaka;
  - (d) mahusiano yao ni ya kutembeleana;
  - (e) mmoja wa wanaodai kuwa wanandoa alifunga ndoa ya mke/mme mmoja na ndoa hiyo inaendelea kutambuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi.
- 3.7.4 Ndoa itakayovunjwa kwa talaka ya mahakama au ya kidini itasitisha na kuondosha haki za:-
- (a) Aliyekuwa mume au mke wa Mwanaumoja;
  - (b) Baba mkwe wa Mwanaumoja; na
  - (c) Mama mkwe wa Mwanaumoja.
- 3.7.5 Iwapo uwepo wa ndoa utatiliwa shaka mwanaumoja atabeba wajibu wa kuthibitisha.
- 3.7.6 Kifo cha Mwanaumoja hakitaathiri huduma kwa mume/mke wake.
- 3.7.7 Mwanaumoja aliyeolewa na Mume ambaye ana mke wa kwanza au wa pili, mke huyo anaweza kujiunga na Umoja.
- 3.7.8 Watoto wa Mwanaumoja waliopatikana nje ya ndoa au ndani ya ndoa kabla au baada ya ndoa hiyo kuvunjika watatambuliwa na kuhudumia kwa uhusiano walionao na mwanaumoja.
- 3.7.9 Mwanaumoja mwenye watoto zaidi ya wanne hawezi kuondoa watoto aliokwisha wajaza kwenye fomu ya taarifa ili ajaze wengine.
- 3.7.10 Wategemezi ambao mwanaumoja hajawajaza kwenye fomu au wamefutwa kwa sababu ya kujaza wengi kuliko idadi inayokubalika kwa mujibu wa katiba hii hawatahudumiwa na Umoja.
- 3.7.11 Mwanaumoja mwenye wake zaidi ya mmoja anaweza kujaza kwenye fomu ya taarifa watoto wa mke ambaye siyo mwanaumoja ili wahudumiwe na Umoja.
- 3.7.12 Mwanaumoja atapewa huduma iwapo:
- (a) Amemaliza miezi sita tangu kujiunga na Umoja; na
  - (b) Hajasimamishwa kupokea huduma kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii;

## SURA YA NNE

### Uanachama kwenye Umoja

4.1 Uanachama kwenye KANONO GROUP umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni:

- (a) Wanaumoja waanzilishi: waliokutana kwa mara ya kwanza na kuanzisha Umoja huu; na
- (b) Wanachama waliojiunga baadaye;

- (c) Wanaumoja waanzilishi na waliojiunga baadaye wote watajulikana kama wanachama au wanaumoja kwa mujibu wa Katiba hii.

4.2 Ili mtu yeyote apokelewe kwenye Umoja sharti awe na sifa zifuatazo:

- (a) umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) Awe amezaliwa, amehamia, ameo au ameolewa Karagwe au Kyerwa;
- (c) mzazi au wazazi wake wamezaliwa, wamehamia, wameoa au wameolewa Karagwe au Kyerwa;
- (d) Mwaminifu;
- (e) Mwenye akili timamu;
- (f) sifa nyingine zilizoainishwa kwenye Kanuni za Umoja; na
- (g) Ni kinyume cha masharti ya katiba hii kwa mtu yeyote anayeishi nje ya mkoa wa Arusha kujiunga na Umoja.

4.3 Kama mwenye kuomba kuwa mwanaumoja alishakuwa mwanaumoja:

- (a) **Kabla ya kupokelewa atalipa madeni aliyoacha kabla ya kuondoka kwenye Umoja;**
- (b) **Kama alifukuzwa kwa sababu za kukiuka taratibu za umoja au kama aliacha madeni atakuwa kwenye kipindi cha majaribio kwa mwaka mmoja; na**
- (c) **Mwanaumoja aliye kwenye kipindi cha majaribio hatapewa huduma yoyote.**

## Kujiunga na Umoja

4.4 Taratibu za Kujiunga na Umoja

4.4.1 Mtu mwenye sifa za kujiunga na Umoja atafuata taratibu zifuatazo:

- (a) atajaza fomu inayopatikana kwa katibu wa kanda eneo analoishi;
- (b) ataweka fedha ya kiingilio kwenye akaunti ya Umoja;
- (c) atapeleka fomu iliyojazwa na bank deposit slip kwa Katibu wa Kanda;
- (d) Viongozi wa Kanda watajadili na kujiridhisha kwamba imejazwa ipasavyo;
- (e) Katibu wa Kanda ataweka maoni ya Kanda; na
- (f) Katibu wa Kanda atapeleka fomu na bank deposit slip kwa Katibu Mkuu wa Umoja.

4.4.2 Baada ya kupokea fomu Katibu Mkuu atajiridhisha na taarifa zifuatazo:

- (a) fomu imejazwa kwa ukamilifu;
- (b) taarifa zilizojazwa hazina mashaka;
- (c) mwombaji ana sifa za kujiunga na Umoja; na
- (d) Iwapo Katibu Mkuu atajiridhisha kwamba fomu imejazwa ipasavyo, ataifikisha kwenye kikao cha Kamati Kuu ili ijadiliwe.

4.4.3 Mtu yeyote atachukuliwa kwamba amepokelewa kwenye Umoja baada ya:

- (a) fomu yake ya maombi ya kujiunga na Umoja kujadiliwa na kikao cha Kamati Kuu na kufikia uamuzi wa kumpokea;
- (b) kupatiwa stakabadhi ya malipo ya kiingilio ambayo uthibitisho wake ni Bank Deposit Slip iliyoambatanishwa kwenye fomu ya maombi ya kujiunga na Umoja.

4.4.4 Mtu atachukuliwa kuwa ni mwanaumoja kuanzia tarehe ya stakabadhi ya malipo ya kiingilio;

4.4.5 Mtu yeyote ambaye maombi yake ya kujiunga na Umoja yamekataliwa kwa sababu za kutoa taarifa za uongo, au uanachama wake umekuwa batili kwa sababu za uongo wakati wa kujaza fomu ya maombi hatarudishiwa fedha aliyokwisha changu kwenye Umoja.

## Haki za Mwanaumoja

### 4.5 Haki za Mwanaumoja

4.5.1 Mwanaumoja wa Kanono Group atakuwa na haki zifuatazo:

- (d) Kuchagua na kuchaguliwa kuwa Kiongozi wa Umoja;
- (e) Kupata taarifa ya mali na fedha za Umoja;
- (f) Kupata taarifa ya mapato na matumizi kila mwezi;
- (d) Kupata taarifa juu ya mwenendo wa shughuli za Umoja;
- (e) Kupewa fursa ya kujitetea mbele ya Kamati ya Nidhamu na Maadili;
- (f) Kupata haki ya kukata rufaa iwapo haridhiki na uamuzi uliotolewa na Kamati ya Nidhamu na Maadili;
- (g) Kushiriki katika shughuli za Umoja;
- (h) Kuhudumiwa katika shida na raha kwa huduma zilizoanishwa kwa mujibu wa katiba hii; na
- (i) Kutoa mawazo kwa uhuru kwenye vikao bila kuzomewa, kutishiwa, kushurutishwa ama kushawishiwa na mtu yeyote ili mradi havunji taratibu za Umoja.

## Wajibu wa Mwanaumoja

### 4.6 Wajibu wa Mwanaumoja

4.6.1 Mwanaumoja wa KANONO GROUP atakuwa na wajibu kama ifuatavyo:

- (a) Kusoma na kuielewa Katiba ya Umoja;
- (b) Kulinda, kutetea na kuheshimu katiba;
- (c) Kulipa ada na michango mingine ndani ya muda;
- (d) Kuunga mkono na kusaidia kwa maneno na vitendo maendeleo ya Umoja;
- (e) Kuhudhuria mikutano, vikao halali na misiba; na
- (f) Shughuli nyingine za Umoja kadri zitakavyoamuliwa na vikao vya Umoja.

## Kukoma kwa Uanachama

4.7 Sababu inazopelekea kukoma kwa Uanachama

4.7.1 Uanachama wa mwanaumoja utakoma kwa sababu ya moja ya mambo yafuatayo:

- (a) Kifo;
- (b) kuthibitika kwamba taarifa zilizomfanya apokelewe kwenye Umoja zilikuwa za uongo;
- (c) Kufukuzwa; na
- (d) Kujiondoa mwenyewe kwa kuandika barua.

4.7.2 Mwanachama anaweza kufukuzwa kwenye Umoja iwapo:

- (a) Atakaidi kutekeleza uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili au uamuzi wa Kamati ya Rufaa kwa zaidi ya miezi mitano;
- (b) Atakaa bila kulipa ada ya Umoja au Kanda kwa muda wa miezi mitano;
- (c) Atashindwa kuhudhuria vikao vinne vya Kanda na vitatu vya Mkutano Mkuu ndani ya mwaka mmoja bila sababu za msingi; na
- (d) Atakataa kulipa mchango halali uliowekwa kwa mujibu wa Katiba hii au kwa uamuzi wa Mkutano Mkuu.

## SURA YA TANO

### Mwanaumoja Kuadhibiwa

#### 5. Utoaji wa adhabu kwenye Umoja

5.1 Mwanaumoja anaweza kuadhibiwa kwa kutozwa faini kwa viwango vilivyoainishwa kwenye kanuni iwapo atatenda makosa yaliyokatazwa kwa mujibu wa Katiba hii.

5.1.1 Mwenyekiti wa kikao au Mkutano anaweza kutoza faini ya papo kwa papo kwa makosa ya:

- (a) kuongea kwenye mkutano au kikao bila ruhusa ya mwenyekiti;
- (b) Kumzomea, kumkatiza kuongea, kutoa lugha ya kashfa au kutoa maneno yenye lengo la kumfanya mtu ashindwe kutoa mawazo yake kwenye kikao au mkutano;
- (c) Kusoma gazeti, kitabu, kuchati au kuongea na simu kwenye kikao au Mkutano; na
- (d) Mwanaumoja kuongea na mwanaumoja mwingine kwenye kikao au Mkutano.

5.1.2 Mwenyekiti wa kikao au Mkutano atatoza adhabu za papo kwa papo kwa:

- (a) Kumweleza mwanaumoja aliyetenda kosa la kuongea kwenye kikao au mkutano;
- (b) Kumweleza mwanaumoja aliyezomea, kutoa lugha ya kashfa au kutoa maneno yenye lengo la kumfanya mtu au mwanaumoja ashindwe kutoa mawazo yake;
- (c) Kumweleza mwanaumoja anayesoma gazeti, kitabu, kuchati au kuongea na simu kwenye kikao au mkutano; na
- (d) Kumweleza mwanaumoja anayeongea na mwanaumoja mwingine wakati kikao au mkutano unaendelea.

5.1.3 Mwenyekiti wa Mkutano au kikao hatachukuliwa kuwa ametenda kosa iwapo:

- (a) Atamkatiza kuongea mwanaumoja au mjumbe wa kikao kwa sababu ya kumpa mwongozo;
- (b) Mwenyekiti atakuwa na jambo la kueleza ili baadaye amruhusu kuendelea kutoa mawazo yake; na
- (c) Mwanaumoja au mjumbe wa kikao ametumia muda mrefu kuongea na hivyo Mwenyekiti kuamua amalizie ili wengine wapate nafasi ya kuchangia.

5.1.4 Adhabu nyingine zitatozwa kwa:

- (a) Kwa Katibu Mkuu kuandaa orodha ya majina ya wanaumoja waliochelewa kwenye Mkutano Mkuu au kutoa pole kwa dakika 15 tangu muda wa kuanza na kuyatangaza kwenye tovuti na/au kuyatuma kwenye Kanda;
- (b) Katibu Mkuu kuandaa orodha ya majina ya wanaumoja ambao hawakuhudhuria mkutano, kutoa pole, au msiba na kuyatangaza kwenye tovuti na/au kuyatuma kwenye Kanda;
- (c) Katibu wa Kanda kuandaa orodha ya wanaumoja ambao mwenyekiti wa Kanda aliwatoza adhabu za papo kwa papo na kuyawasilisha kwa Katibu Mkuu;
- (d) Katibu wa Kanda kuandaa orodha ya wanaumoja waliochelewa kwenye kikao cha kanda zaidi ya 15 na kuyawasilisha kwa Katibu Mkuu; na
- (e) Katibu wa Kanda kuandaa orodha ya Wanaumoja ambao hawakuhudhuria Kikao cha Kanda na kuyawasilisha kwa Katibu Mkuu.

5.1.5 Mwanaumoja atawajibika kulipa adhabu zinazotokana na vikao ndani ya miezi mitatu kuanzia tarehe ya kutenda kosa ambalo anaadhibiwa.

- 5.1.6 Mwanaumoja anaweza kufikishwa mbele ya Kamati ya Nidhamu kwa makosa ya:
  - (a) Kutohudhuria mfululizo vikao vitatu vya Kanda bila ruhusa;
  - (b) Kutohudhuria Mkutano Mkuu mara mbili mfululizo;
  - (c) Kutoa lugha ya matusi kwa kiongozi yeyote; na
  - (d) Kudharau wito wa Kamati ya Nidhamu na Maadili.
- 5.1.7 Adhabu inayotokana na vikao vya kushughulikia nidhamu italipwa ndani ya muda ulioamuriwa na kikao husika.
- 5.1.8 Kamati Kuu inawajibika kutekeleza uamuzi unaotolewa na vikao vya kushughulikia nidhamu kwenye Umoja.

### ***Mwanaumoja Kusimamishwa Huduma***

- 5.1.9 Mwanaumoja atahesabiwa kwamba amesimamishwa huduma iwapo:
  - (a) Anadaiwa ada ya Umoja sawa na miezi mitatu;
  - (b) Anadaiwa ada ya Kanda sawa na miezi mitatu;
  - (c) Anadaiwa harambee baada ya tarehe ya mwisho ya kulipa;
  - (d) Anadaiwa mchango wa kutunisha baada ya tarehe ya mwisho ya kulipa;
  - (e) Anadaiwa adhabu ya papo kwa papo baada ya tarehe ya mwisho ya kulipa; na
  - (f) Anadaiwa adhabu aliyotowza na Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Rufaa baada ya muda wa mwisho wa kulipa kuisha.
- 5.1.10 Mwanaumoja aliyesimamishwa huduma:
  - (a) Atawajibika kuendelea kutekelaza wajibu kwa kulipa ada ya Umoja na kanda, kutunisha, harambee, kuhudhuria vikao vya kanda, mkutano mkuu, misiba, kutoa pole na majukumu mengine yenye kufanana na hayo; na
  - (b) Atarudishiwa huduma mwezi mmoja baada ya kulipa deni lililosababisha afungiwe huduma.
- 5.1.11 Mwanaumoja aliyesimamishwa huduma au uanachama hatapewa huduma kwa tukio lililomkuta ndani ya muda ambao atakuwa amefungiwa huduma au kusimamishwa uanachama.

### **Utaratibu wa Kumfukuza Mwanaumoja**

- 5.2 Umoja utafuata utaratibu ufuatao kumfukuza Mwanaumoja:
  - 5.2.1 Kamati Kuu itaandaa azimio ambalo litaainisha makosa anayotuhumiwa Mwanaumoja;
  - 5.2.2 Azimio litawasilishwa kwenye Kikao cha Halmashauri kujadiliwa na kupigiwa kura ya siri;
  - 5.2.3 Mwanaumoja ambaye azimio limeandaliwa dhidi yake ataalikwa kufika mbele ya Halmashauri kutoa utetezi wake;
  - 5.2.4 Baada ya utetezi wake Mwanaumoja ataondoka kwenye kikao ili kutoa nafasi ya kumjadili;
  - 5.2.5 Baada ya kumjadili Wanaumoja watapiga kura ya siri ya kuamua iwapo afukuzwe; na
  - 5.2.6 Iwapo wajumbe wa Halmashauri walio wengi wameamua mwanaumoja afukuzwe, mwanaumoja huyo atahesabika kuwa amefukuzwa.
- 5.3 Mwanaumoja ambaye Kikao cha Halmashauri kimepitisha uamuzi wa kumfukuza anaweza:

- 5.3.1 kukata rufaa kwenye Mkutano Mkuu, kupinga uamuzi wa Halmashauri, ndani ya siku 28 tangu kupokea barua ya kumfukuza;
- 5.3.2 kuomba Halmashauri kurejea uamuzi wake kwa kuainisha makosa ya kiufundi ambayo kama yasingekuwepo Halmashauri isingefikia uamuzi wa kumfukuza; na
- 5.3.3 Mwanaumoj ambaye Halmashauri imefikia uamuzi wa kumfukuza, hataomba rufaa Mkutano Mkuu au kuomba Halmashauri kurejea uamuzi wake iwapo hakuitika wito wa kufika kujitetea mbele ya Halmashauri bila sababu za msingi.

### **Utaratibu wa Kupeleka Mashauri Mbele ya Kamati ya Nidhamu Na Maadili**

- 5.4 Kupeleka mashauri mbele ya Kamati ya Nidhamu na Maadili kutafuata masharti yaliyowekwa na Katiba hii.
  - 5.4.1 Kamati ya Nidhamu na Maadili haitashughulikia shauri lolote isipokuwa:
    - (a) lililofikishwa mbele yake na Katibu Mkuu;
    - (b) lililofikishwa mbele yake na Katibu Mkuu kwa maombi ya Mwanaumoj ambaye madai dhidi ya mwanaumoj mwenzake;
    - (c) lililofikishwa na Katibu Mkuu kwa maombi ya uongozi wa Kanda; na
    - (d) lililofikishwa na Katibu Mkuu kwa kosa lolote dhidi ya mwanaumoj ilimradi kosa hilo linaathiri Umoja kwa namna moja au nyingine.

### **Utaratibu wa kushughulikia Mashauri**

- 5.4.2 Katika kushughulikia mashauri, Kamati ya Nidhamu na Maadili:
  - (a) Itamwalika mwanaumoj anayelalamikiwa;
  - (b) Itamsomea na kumweleza kwa ufasaha makosa anayotuhumiwa nayo;
  - (c) Mwanaumoj atatoa utetezi wake wa maandishi kwenye fomu maalum;
  - (d) Kwa kuzingatia utetezi wake wa maandishi, kamati itamhoji na kuhitaji ufafanuzi wa hoja alizoibua kwenye utetezi wake;
  - (e) Kama atakutwa na makosa Kamati itamuamuru kulipa adhabu;
  - (f) Kamati ya Nidhamu na Maadili itawajibika kuandika uamuzi ambao:
  - (g) Mlalamikaji atapewa nakala halisi;
  - (h) Mlalamikiwa atapewa nakala halisi;
  - (i) Katibu Mkuu atapewa nakala;
  - (j) Katibu wa Kanda atapewa nakala; na
  - (k) Nakala itahifadhiwa kwenye faili la Kamati ya Nidhamu na Maadili.
- 5.4.3 Katika kutoza adhabu Kamati ya Nidhamu na Maadili itazingatia:
  - (a) Uzito wa makosa yanayomkabili mwanaumoj;
  - (b) Kujirudia kwa makosa yaleyale;
  - (c) Lugha ya matusi kwa wajumbe wa Kamati; na
  - (d) Kutotii wito wa Kamati.

### **Kukata Rufaa**

- 5.5 Katika kukata Rufaa, mkata rufaa atazingatia masharti yaliyoainishwa na Katiba.
  - 5.5.1 Upande wowote kwenye shauri unaweza kukata rufaa kwenda Kamati ya Rufaa iwapo hautaridhika na uamuzi uliotolewa na Kamati ya Nidhamu na Maadili kwa:

- (a) Kuwasilisha kwa Katibu wa Kamati ya Rufaa kwa maandishi na nakala upande mwingine katika shauri akieleza sababu za kutoridhika na uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili ndani ya siku nane toka alipopokea uamuzi anaoukatia rufaa;
- (b) Katika kukata rufaa asiibue mambo mapya ambayo hayakuibuliwa wakati shauri likiwa mbele ya Kamati ya Nidhamu na Maadili; na
- (c) Rufaa iliyowasilishwa nje ya muda bila sababu za msingi haitapokelewa.

### **Usikilizaji wa Rufaa**

- 5.5.2 Katika kushughulikia rufaa Kamati ya Rufaa:
  - (a) Itajiridhisha iwapo Kamati ya Nidhamu na Maadili ilishindwa kuzingatia hoja za msingi alizozisimamia mlalamikaji;
  - (b) Itajiridhisha iwapo mlalamikaji hakustahili kuadhibiwa kwa makosa ambayo Kamati ya Nidhamu ilimkuta nayo; na
  - (c) Iwapo rufaa ni ya kupinga ukubwa wa adhabu, Kamaati tajiridhisha iwapo adhabu iliyotolewa na Kamati ya Nidhamu na Maadili ni kubwa ikilinganishwa na makosa anayolalamikiwa.
- 5.5.3 Iwapo Kamati ya Rufaa itajiridhisha kwamba Kamati ya Nidhamu na Maadili ilifanya makosa katika kufikia uamuzi wake inaweza:
  - (d) kuubatilisha;
  - (e) Inaweza kuurekebisha; na
  - (f) Inaweza kumpa nafuu anayoweza kuwa anastahili.
- 5.5.4 Kamati ya Rufaa ikijiridhisha kwamba Kamati ya Nidhamu na Maadili haikufanya kosa lolote katika kufikia uamuzi au makosa yaliyofanywa hayatoshi kuubatilisha uamuzi:
  - (a) Kamati ya Rufaa itatupilia mbali mbaombi ya mkata rufaa;
  - (b) Itamuamuru atekeleze uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili Kama ulivyo; na
  - (c) Inaweza kumuamuru alipe gharama za kikao cha Kamati ya Rufaa .
- 5.5.5 Uamuzi wa Kamati ya Rufaa utakuwa wa mwisho.

## **SURA YA SITA**

### **Mfuko wa Umoja:**

- 6.1 Mfuko wa Umoja utakuwa na maana ya Mfuko Mkuu wa Umoja na Mfuko wa Kanda:

### **Vyanzo vya Mapato vya Mfuko Mkuu**

- 6.1.1 Vyanzo vya mapato vya Mfuko Mkuu wa Umoja ni:
  - (a) Viingilio vya kujiunga na Umoja;
  - (b) Ada ya Umoja ya kila mwezi;
  - (c) Adhabu za papo kwa papo;
  - (d) Adhabu zinazotokana na uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili na Kamati ya Rufaa;
  - (e) Kutunisha;



- (f) Harambee;
- (g) Mnada;
- (h) Faida itokanayo na mikopo;
- (i) Faida itokanayo na uwekezaji;
- (j) Misaada kutoka kwa watu binafsi au taasisi; na
- (k) Vyanzo vingine vya mapato.

### **Masharti yatakayotawala malipo na matumizi ya Mfuko Mkuu**

6.1.1.1 Masharti yafuatayo yatatawala uwekaji na matumizi ya fedha ya mfuko mkuu wa Umoja:

- (a) Fedha yote iliyokusanywa kwa ajili ya mfuko mkuu itawekwa kwenye akaunti za hundi zilizofunguliwa kwenye benki zilizokubaliwa kwenye Mkutano Mkuu;
- (b) Malipo yote yatakatiwa stakabadhi ambayo pekee ndiyo uthibitisho wa malipo;
- (c) Malipo yatahesabika kuwa yamefanyika baada ya kupokea stakabadhi ya Umoja;
- (d) Hela itatolewa kwenye akaunti kwa watia saini wawili kati ya watatu kusaini hundi;
- (e) Watia saini kwenye hundi watateuliwa na Halmashauri ya Umoja; na
- (f) Watia saini kwenye hundi wawe wanaumoja wanaoweza kupatikana kwa urahisi.

### **Mazingira yanayoruhusiwa kupokea Fedha Taslim**

6.1.1.2 Viongozi wanaruhusiwa kupokea fedha taslimu inayotokana na:

- (a) Mnada na ambayo imelipwa wakati mnada unaendelea au mara tu baada ya kumalizika;
- (b) Harambee wakati inaendelea au mara tu baada ya kumalizika;
- (c) Malipo yoyote yaliyofanywa na mtu ambaye siyo mwanaumoja;
- (d) Zawadi iliyotolewa papo hapo; na
- (e) Fedha nyingine ambayo itapokelewa kwa mazingira yaliyoruhusiwa na Halmashauri.

6.1.1.3 Bila kuathiri vifungu vingine vya katiba, itakuwa kinyume cha masharti ya Katiba hii kwa:

- (a) Mwanaumoja yeyote kulipa fedha taslim kwa kiongozi; na
- (b) Kiongozi yeyote kupokea fedha taslim kutoka kwa mwanaumoja yeyote.

6.1.1.4 Kiongozi atakayekiuka katazo la kupokea fedha taslim:

- (a) Atakuwa ametenda kosa;
- (b) Atafikishwa mbele ya Kamati ya Nidhamu na Maadili; na
- (c) Atawajibika kutekeleza uamuzi wa Kamati ya Nidhamu.

### **Taarifa ya Mapato na Matumizi**

6.1.1.5 Mweka Hazina ataandaa taarifa ya mapato ikihusisha fedha yote iliyopatikana kutokana na:

- (a) Ada ya Umoja ya kila mwezi;
- (b) Kila adhabu;

- (c) Harambee;
- (d) Kutunisha;
- (e) Viingilio;
- (f) Faida inayotokana na kuweka fedha benki;
- (g) Faida inayotokana na kuwekeza kwenye SACCOS; na
- (h) Vyanzo vingine.

6.1.1.6 Mweka Hazina ataandaa taarifa ya matumizi ikihusisha:

- (a) Matumizi ya vikao na mikutano ya Umoja;
- (b) matumizi kwa kila huduma;
- (c) gharama za benki;
- (d) gharama za ukaguzi wa hesabu; na
- (e) matumizi mengine.

#### ***Ukaguzi wa Mapato na Matumizi ya Mfuko Mkuu***

6.1.1.7 Mwaka wa fedha wa Umoja unaanza tarehe 1 Julai na kuisha tarehe 30 Juni kila mwaka.

6.1.1.8 Hesabu za Umoja zitakaguliwa na taarifa kutolewa na wakaguzi wenye taaluma ya ukaguzi kutoka aidha miongoni mwa wanaumoja au nje ya Umoja:

- (a) Ndani ya miezi mitatu tangu kufunga mwaka wa fedha;
- (b) Wakaguzi watakabidhi taarifa kwa Kamati Kuu mara tu baada ya kumaliza kukagua;
- (c) Kamati Kuu itawasilisha taarifa ya ukaguzi kwenye kikao cha kawaida cha Halmashauri au cha dharura ili wakaguzi wawasilishe taarifa ya ukaguzi na kuifafanua;
- (d) Halmashauri itaijadili kwa kina kabla ya kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Septemba.

#### ***Kima cha Chini cha Mfuko Mkuu na Matumizi yake***

6.1.1.9 Muda wowote ule mfuko wa Umoja utakuwa na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Mkutano Mkuu kuwa kima cha chini. Fedha itahesabika kuwa ni sehemu ya fedha iliyopo kwenye mfuko wa Umoja iwapo:

- (a) Ipo kwenye akaunti za Umoja;
- (b) Ipo kwenye mikopo ya muda mfupi; na
- (c) Imewekezwa kwenye SACCOS kama Amana.

6.1.1.10 Mfuko mkuu wa Umoja utatumika kwa mambo yafuatayo:

- (a) Kutoa huduma zilizoainishwa na katiba hii na viwango vyake kutajwa kwenye kanuni;
- (b) Kugharimia vikao vya Umoja na uendeshaji wa Umoja;
- (c) Uwekezaji kwenye SACCOS; na
- (d) Uwekezaji kwenye miradi.

## Mfuko wa Kanda

6.1.2 Mfuko wa Kanda utakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo:

- (a) Ada ya kanda ya kila mwezi ambayo imeidhinishwa na Kamati Kuu kwa maandishi; na
- (b) Mchango mwingine ambao kanda itaomba kwa maandishi na Kamati Kuu kuuidhinisha kwa maandishi.

6.1.2.1 Ada ya kanda ya kila mwezi:

- (a) Haitawekwa kwenye akaunti ya mfuko mkuu wa Umoja; na
- (b) Itatumika kwa ajili ya matumizi madogomadogo ya Kanda kadiri yatakavyoainishwa na kanuni.

## Mikopo kwenye Umoja

6.2 Mikopo kwenye Umoja

6.2.1 Umoja utatoa mikopo midogomidogo kwa wanaumoja kwa masharti yafuatayo:

- (a) Muda wa kulipa mkopo na riba yake ni miezi minne;
- (b) Mkopo utarejeshwa katika marejesho manne kwa utaratibu wa kurejesha kila mwezi 25% au zaidi ya mkopo wote pamoja na riba; na
- (c) Mkopo utatozwa riba ya asilimia 10 kwa kipindi chote cha miezi minne.

6.2.2 Mkopo hautatolewa mpaka:

- (a) Mwanaumoja awe ametimiza miezi sita tangu kujiunga na Umoja;
- (b) Mkopaji awe amejaza fomu ya maombi ya mkopo na kudhaminiwa na wadhamini wasiopungua wawili;
- (c) Kamati Kuu iwe imejiridhisha kwamba mkopaji hajawahi kushindwa kulipa mkopo;
- (d) Kama aliwahi kushindwa kulipa mkopo ithibitike kwamba alishalipa hela ya wadhamini ambayo walimlipia kwa mkopo alioshindwa kurejesha;
- (e) Mkopaji na wadhamini wake wawe wanaumoja hai; na
- (f) Awe na uwezo wa kurejesha.

## Kucheleweshwa Mkopo

6.2.3 Atakayecheleweshwa mkopo:

- (a) atatozwa adhabu ya asilimi 10 ya mkopo wote pamoja na riba yake iwapo atalipa ndani ya siku thelathini tangu muda wa kawaida wa kulipa mkopo kuisha;
- (b) mweka Hazina atawajulisha wadhamini wa mkopaji baada ya mkopo kucheleweshwa siku 10;
- (c) mkopaji na wadhamini watawajibika kulipa mkopo, riba na adhabu ndani ya siku 30 tangu muda wa kawaida wa kulipa kuisha;
- (d) siku 30 zikiisha bila kulipa mkopo mkopaji na wadhamini watafungiwa huduma;

## Kushindwa kulipa Mkopo

6.2.4 Iwapo wadhamini watalipa mkopo kabla au baada ya kufungiwa huduma:

- (a) kwa maombi ya wadhamini mkopaji ataendelea kufungiwa huduma;
- (b) kwa maombi ya wadhamini atafikishwa Kamati ya Nidhamu na Maadili; na
- (c) kama mkopaji ni kiongozi atapoteza nafasi yake ya uongozi baada ya wadhamini kuomba aendelee kufungiwa huduma.

## **SURA YA SABA:**

### **Vikao vya Umoja na Majukumu yake**

#### **Mkutano Mkuu**

- 7.1.1 Mkutano Mkuu utakuwa ni mkutano wa Wanaumoja wote ambao ndicho chombo cha juu kabisa cha maamuzi katika Umoja.
- 7.1.2 Wajumbe wa Mkutano Mkuu ni Wanaumoja wote wa “Kanono Group”
- 7.1.3 Mkutano Mkuu utafanyika mara moja kwa miezi mitatu.
- 7.1.4 Mkutano Mkuu utaitishwa Jumapili ya nne ya miezi ya Machi, Juni, Septemba na Juma pili ya kwanza ya mwezi Disemba kila mwaka kwa utaratibu wa kuzunguka kwenye Kanda.
- 7.1.5 Akidi ya Mkutano Mkuu ni asilimia 60 ya Wanaumoja wote.
- 7.1.6 Mkutano Mkuu wa dharura utaitishwa kwa uamuzi ya Halmashauri endapo kutakuwepo na jambo lolote la dharura linalohitaji uamuzi wa Mkutano Mkuu.
- 7.1.7 Akidi ya Mkutano wa dharura ni asilimia 40 ya Wanaumoja wote.
- 7.1.8 Mkutano Mkuu utanza saa tisa alasiri na kumalizika saa kumi na mbili jioni.
- 7.1.9 Kwa ridhaa ya wajumbe walio wengi dakika 15 kabla ya muda wa kawaida wa vikao kuisha, mwenyekiti anaweza kuongeza hadi dakika 30 kumalizia agenda zilizobaki.
- 7.1.10 Katibu Mkuu ataandaa ratiba ya mzunguko wa Mkutano Mkuu kwenye Kanda na kutoa nakala kwa makatibu wa kanda zote.
- 7.1.11 Mwanaumoja mwenyeji wa Mkutano Mkuu hawajibiki, ila kwa hiari yake, kuwahudumia wajumbe kwa vinywaji au chakula.
- 7.1.12 Kiasi cha fedha kitakachoinishwa kwenye Kanuni za Umoja kitatolewa kutoka mfuko wa Umoja kwa ajili kugharimia Mkutano Mkuu.

#### **Njia itakayotumika kuwaalika Wajumbe wa Mkutano Mkuu**

- 7.1.13 Ujumbe mfupi wa simu za mikononi (SMS) utatumika kuwaalika Wajumbe wa Mkutano Mkuu baada ya Mwenyekiti na Katibu Mkuu kushauriana.
- 7.1.14 Katika kuwaalika wanaumoja kwenye Mkutano Mkuu yafuatayo yatazingatiwa:
  - (a) Katibu wa Mkutano au kikao atatuma ujumbe mfupi wa simu kwa wajumbe wote wa mkutano aidha kupitia kwa viongozi wa Kanda au kwa njia nyingine ifaayo;
  - (b) Ujumbe utakuwa na taarifa za kutosha kuhusu mkutano au kikao kwa kutaja waalikwa, muda wa kikao, tarehe, siku, mahali pa kukutana, maelekezo ya kufika eneo la kukutana, jina la mwandishi anayetuma mwaliko, cheo chake, mawasiliano muhimu iwapo mjumbe atahitaji kuelekezwa zaidi; na maelezo mengine kadri itakavyo onekana inafaa.
  - (c) iwapo Mkutano ni wa dharura, agenda itajwe kwenye SMS ya mwaliko.

## Namna ya kutuma Ujumbe wa Mwaliko

- 7.1.15 Ujumbe mfupi wa simu wa mwaliko wa mkutano au taarifa nyingine utakapotumwa bila kupoteza muda viongozi wa Kanda watawajibika:-
- (a) Kama ujumbe una mapungufu kuwasiliana na mwandishi mara moja ili arekebishe mapungufu hayo;
  - (b) Kutuma ujumbe huo mara moja kwa wanaumoja wote wa Kanda husika; na
  - (c) Kujiridhisha kwamba kila mwanaumoja kwenye Kanda amepata ujumbe huo.
- 7.1.16 Ili mamlaka inayoalika au kutoa taarifa ibakie ileile na ili ujumbe ubakie wa mwandishi; na ili ujumbe uwafikie wanaumoja wote kama mwandishi alivyolenga viongozi wa Kanda wanakatazwa-
- (a) kuufanyia marekebisha ya aina yoyote ile isipokuwa yale yasiyobadilisha maudhui kama ya kiuchapishaji (typing error);
  - (b) katazo hili haliwazuii viongozi wa Kanda au Kamati za kikatiba kuandika na kutuma ujumbe kwa wanaumoja wanaowaongoza ili kufikisha mwaliko wa vikao vya ngazi zao, kuhamasisha juu ya masuala mbalimbali au kusisitiza jambo lililoagizwa kwenye ujumbe uliopokelewa kutoka uongozi wa juu.

## Majukumu ya Mkutano Mkuu

- 7.1.17 Mkutano Mkuu utakuwa na majukumu yafuatayo:
- (a) Kupokea na kujadili taarifa ya hali ya Umoja, Kanda na Kamati za kikatiba kwa kipindi cha miezi mitatu;
  - (b) Kupokea na kujadili taarifa ya fedha ya miezi mitatu;
  - (c) Kutoa maelekezo/madaraka kwa Halmashauri na Kamati Kuu kwa masuala mahsusi kadri utakavyoona inafaa ilimradi isiwe kinyume cha Katiba ya Umoja;
  - (d) Bila kuathiri masharti ya Katiba, kuchagua Viongozi wa Kamati Kuu na Wajumbe wa Kamati za kikatiba;
  - (e) Kupitisha mabadiliko ya Katiba.
  - (f) Kuwafukuza viongozi wa Kamati Kuu waliothibitika kutenda kinyume cha Katiba, maadili ya kijamii na walioshindwa kutekeleza majukumu yanayoambatana na nafasi wanazozitumikia.

## Halmashauri

### 7.2 Halmashauri ya Umoja

- 7.2.1 Halmashauri ni chombo ambacho kitapokea mapendekezo yaliyojadiliwa na Kamati Kuu.
- 7.2.2 Kwa minajili ya uwajibikaji wa pamoja (collective responsibility) na uhifadhi wa siri za vikao, wajumbe wa Halmashauri wanawajibika kulinda na kutetea maamuzi yaliyofikiwa

hata kama kuna mjumbe asiyeunga mkono maamuzi hayo ilimradi maamuzi wanayoyatetea:

- (a) siyo kinyume cha masharti ya Katiba hii;
- (b) hayalengi kuzuia haki kutendeka;
- (c) hayakiuki misingi ya umoja na mshikamano katika Umoja; na
- (d) hayana misingi ya ubaguzi ubaguzi.

### **Vikao vya Halmashauri**

- 7.2.3 Wajumbe wa kikao cha Halmashauri watakuwa ni wajumbe wote wa Kamati Kuu, wenyeviti wa Kanda na wenyeviti wa Kamati za kikatiba. Kamati ya wazee haitakuwa na uwakilishi kwenye Halmashauri.
- 7.2.4 Kikao cha Halmashauri kitakaa mara moja kwa miezi miwili.
- 7.2.5 Kikao cha Halmashauri kitafanyika Jumapili ya tatu ya mwezi Agosti, Ocktoba, Februari, Aprili, Juni na Jumapili ya mwisho ya mwezi Novemba.
- 7.2.6 Halmashauri inaweza kufanya kikao cha dharura wakati wowote iwapo kutajitokeza suala lolote linalohitaji uamuzi wa haraka.
- 7.2.7 Kikao cha Halmashauri kinaweza kufanyika mahali popote ambako sio nyumbani kwa Mjumbe wa Halmashauri kadri Wajumbe watakavyoona inafaa kwa gharama za mfuko wa Umoja.

### **Majukumu ya Halmashauri**

- 7.2.8 Halmashauri ya Umoja itakuwa na Majukumu yafuatayo:-
  - (a) Kupokea na kujadili taarifa ya Kamati Kuu juu ya hali ya Umoja, Kanda, na Kamati za kikatiba;
  - (b) Kupokea na kujadili taarifa ya fedha kwa kipindi cha miezi miwili;
  - (c) Kutoa maelekezo/madaraka kwa Kamati Kuu kwa masuala mahsusi ilimradi hayaendi kinyume na masharti ya Katiba na sheria za nchi;
  - (d) Kusimamia utekelezaji wa maagizo na maelekezo ya Mkutano Mkuu;
  - (e) Kujadili mafanikio na matatizo ya Kamati Kuu, Kanda na Kamati za kikatiba;
  - (f) Kujadili masuala ya jumla yatakayozingatiwa na Kamati Kuu wakati wa kuandaa taarifa itakayowasilishwa na Kamati Kuu kwenye Mkutano Mkuu.
  - (g) Kujadili na kupitisha Kanuni za Umoja ambazo zitawezesha utekelezaji bora wa Katiba.
- 7.2.9 Katika kujadili na kupitisha kanuni au mabadiliko ya Kanuni, Halmashauri itazingatia:
  - (a) Rasimu iliyowasilishwa mbele yake na Kamati ya Katiba;
  - (b) Ufafanuzi wa Kamati ya Katiba uliotokana na utafiti;
  - (c) Maslahi mapana ya Umoja;
  - (d) Utekelezaji bora wa Katiba; na
  - (e) Uendeshaji bora wa shughuli za Umoja.
- 7.2.10 Kujadili na kutoa uamuzi wa kuwafukuza na kuwafuta kwenye daftari la wanachama wanaumoja waliokiuka masharti ya Katiba.

7.2.11 Kuagiza Mkutano Mkuu wa dharura uitishwe iwapo kuna jambo la lazima ambalo linahitaji uamuzi wa Mkutano Mkuu. Iwapo Halmashauri imeamuru kuitishwa kwa Mkutano Mkuu, Mwenyekiti na Katibu Mkuu watawajibika:

- (a) Kuitisha Mkutano Mkuu wa dharura ndani ya siku 10;
- (b) Kutuma ujumbe wa mwaliko ndani ya masaa 48 tangu Halmashauri kupitisha uamuzi wa kuitisha Mkutano Mkuu wa Dharura;
- (c) Kwenye ujumbe wa simu wa mwaliko kutaja eneo la kukutana ambalo limekubaliwa na Kikao cha Halmashauri, muda wa kuanza mkutano na agenda;

7.2.12 Kuwajadili viongozi wa Kamati Kuu ambao:

- (a) Wameshindwa kutekeleza wajibu wao;
- (b) Wametenda kinyume cha maadili ya uongozi;
- (c) Wamepoteza sifa za kuwa viongozi; na
- (d) Wamefuja mali za Umoja.

7.2.13 Katika kumjadili kiongozi Halmashauri itazingatia:

- (a) Kusoma kwa ufasaha tuhuma zinazomkabili kiongozi;
- (b) Kutoa nafasi ya kujitetea kwa kiongozi anayetuhumiwa;
- (c) Kumwamuru kiongozi anayejadiliwa kuondoka kwenye kikao kinachomjadili mara baada ya kutoa utetezi wake;
- (d) Haki, utu wa kiongozi anayejadiliwa na maslahi mapana ya Umoja;
- (e) Masharti ya Katiba hii na Kanuni za Umoja;
- (f) Utetezi wa kiongozi;
- (g) Kuamua iwapo kiongozi anayejadiliwa amekutwa na makosa; na
- (h) Kuainisha na kumweleza makosa ambayo kiongozi amekutwa nayo.

7.2.14 Iwapo Halmashauri imemkuta kiongozi ana hatia inaweza:

- (a) Kumshauri ajirekebishe ili aendane na taratibu za Umoja;
- (b) Kumshauri ajiuzulu nafasi yake;
- (c) Kumwandikia barua ya kumshauri ajiuzulu nafasi yake; au
- (d) Kupendekeza kwa Mkutano Mkuu aondolewe kwenye uongozi.

7.2.15 Kumjadili kiongozi wa Kanda kwa makosa aliyoyatenda. Iwapo Halmashauri itamkuta na makosa inaweza:

- (a) Kumshauri ajirekebishe;
- (b) Kutoa maelekezo kwa Katibu Mkuu amwandikie barua ya onyo;
- (c) Kumshauri ajiuzulu nafasi yake; na
- (d) Kuagiza Kanda yake imvue uongozi na kuchagua mwingine.

## **Kamati Kuu**

### **7.3 Kamati Kuu ya Umoja**

- 7.3.1 Kamati Kuu ni chombo cha utekelezaji wa masuala yote yatakayopitishwa na Halmashauri na Mkutano Mkuu wa Umoja.
- 7.3.2 Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati Kuu inawajibika kusimamia Kamati za Kikatiba, Kanda na Wanaumoja kwa ujumla.

### Vikao vya Kamati Kuu

- 7.3.3 Kamati Kuu itakutana kila mwezi:-
  - (a) siku yoyote inayofaa kabla au kwenye wiki ya pili ya mwezi
  - (b) Kamati Kuu inaweza kukutana kwa dharura itakapolazimika kufanya hivyo ilimradi isiwe zaidi ya kikao kimoja cha dharura ndani ya mwezi mmoja.
  - (c) Kikao cha Kamati Kuu kinaweza kufanyika mahali ambapo Wajumbe wataona panafaa lakini isiwe nyumbani kwa mtu.

### Majukumu ya Kamati Kuu

- 7.3.4 Kamati Kuu itakuwa na majukumu yafuatayo:-
  - (a) Kuhakikisha unakuwepo umoja na mshikamano kwenye Umoja.
  - (b) Kusimamia maendeleo na kutoa miongozo ya utendaji kwenye Kanda na Kamati za Kikatiba
  - (c) Kusimamia utekelezaji wa Kanuni, katiba na kuhakikisha ustawi wa Umoja kwa ujumla.
  - (d) Kuratibu shughuli za kila siku za Umoja
  - (e) Kuhamasisha watu wenye sifa kujiunga na Umoja
  - (f) Kusimamia mapato na matumizi ya Umoja na Kanda
  - (g) kusimamia nidhamu ya Wanaumoja katika kufuata taratibu tulizojiwekea;
  - (h) Kuhamasisha ulipaji wa ada na michango
  - (i) Kuratibu shughuli zote za Umoja
  - (j) Kutoa taarifa kwa Wanaumoja ili mradi taarifa hizo haziathiri malengo na madhumuni ya Umoja.
  - (k) Kumwongezea majukumu madogo madogo kiongozi yeyote kwa jinsi itakavyoona inafaa ili akaimu nafasi ya kiongozi ambayo iko wazi au mwenye kuishikilia ana udhuru unaomfanya asiweze kutekeleza majukumu yake;
  - (l) Baada ya kumwongezea majukumu kiongozi, Kamati Kuu itawajulisha wanaumoja aidha kupitia viongozi wa Kanda au vikao vya Umoja; na
  - (m) Kusimamia nidhamu na utendaji wa viongozi wa Kanda.
- 7.3.5 Kwa kushirikiana na Kanda, pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii:-
  - (a) kuratibu shughuli na matukio yanayotambuliwa na katiba;
  - (b) kuandaa na kuratibu sherehe ya Ka-Nono Day;
  - (c) Kuratibu tukio la kutoa pole; na
  - (d) Masuala mengine kadri yatakavyoainishwa na Kanuni.
- 7.3.6 Kwa kushirikiana na Kamati ya Nidhamu na Maadili:



- (a) Kushughulikia masuala yanayohusiana na nidhamu ya wanaumoja;
- (b) Kusimamia uwajibikaji kwenye Umoja;
- (c) Kusimamia viongozi wa Kanda; na
- (d) Kusimamia viongozi wa Kamati za Kikatiba.

7.3.7 Kwa kushirikiana na Kamati ya Fedha na Uchumi:-

- (a) kubuni na kuibua fursa mbali mbali za maendeleo ya Umoja;
- (b) kubuni na kuibua miradi mbali mbali ya Umoja;
- (c) kutathimini maendeleo ya Umoja kiuchumi;
- (d) kuchukua hatua kwa nia ya kujikwamua na kujitegemea kiuchumi; na
- (e) Kusimamia masuala yanayohusiana na fedha kwenye Kanda.

## **Kamati za Kikatiba**

### 7.4 Kamati za Kikatiba

7.4.1 Kutakuwepo na Kamati saba za kikatiba. Kamati hizi ni zifuatazo:-

- (a) Kamati ya Nidhamu na Maadili;
- (b) Kamati ya Rufaa;
- (c) Kamati ya Fedha na Uchumi;
- (d) Kamati ya Huduma za Jamii;
- (e) Kamati ya Wazee;
- (f) Kamati Maalum; na
- (g) Kamati ya Katiba.

7.4.1.1 Majukumu yote ya Umoja ambayo ni ya kawaida na yasiyokuwa ya kawaida yatagawanywa kwa uwiano unaofaa kwa Kamati za Kikatiba.

7.4.1.2 Iwapo idadi ya wajumbe wa kamati itakuwa ndogo kiasi cha kuathiri ufanisi wa Kamati katika kutekeleza jambo lolote:-

- (a) Kamati kuu inaweza kuteua wanaumoja kwa idadi ifaayo ili kuongezea kamati uwezo wa rasilimali watu;
- (b) wanaumoja walioteuliwa na Kamati Kuu watakuwa wajumbe wa Kamati husika kwa kipindi ambacho shughuli waliyoteuliwa kufanya itakuwa haijamalizika;

7.4.1.3 Kamati Kuu isipowaongezea muda, ujumbe wao kwenye Kamati utakoma mara baada ya majukumu waliyopewa kumalizika. Kamati za kikatiba zitazingatia yafuatayo katika kufanya vikao vyake:-

- (a) Kamati haitakuwa na vikao endapo hakuna kazi inayoilazimu kukutana;
- (b) Kamati itakutana kwa wito wa Katibu wa Kamati baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Kamati;
- (c) Kama mwenyekiti wa kamati hayupo, wajumbe wataamchagua mmoja wao kuongoza kikao cha kamati. Mwenyekiti wa muda atokane na wajumbe wa kuchaguliwa;
- (d) Kama Katibu wa Kamati hayupo, Mweka Hazina wa kamati atakaimu nafasi ya katibu;
- (e) Iwapo Katibu wa Kamati na Mweka Hazina wa Kamati wote hawapo, mjumbe yeyote lakini siyo Mwenyekiti wa Kamati atachaguliwa na wajumbe kukaimu nafasi ya Katibu wa Kamati;
- (f) Kamati za kikatiba hazitafanya vikao nyumbani kwa mtu; na

- (g) Kamati itakuwa huru kufanya vikao vyake saa yoyote kwa mujibu wa makubaliano ya Wanakamati kufuatana na majukumu yanayowakabili.

## **Kamati ya Nidhamu na Maadili**

### **7.4.2 Kamati ya Nidhamu na Maadili**

#### **7.4.2.1.1 Kamati ya Nidhamu na Maadili itakuwa na Majukumu yafuatayo:-**

- (a) Kushughulikia mashauri yote ya nidhamu yatakayopelekwa mbele yake na Katibu Mkuu;
- (b) kuelekeza hatua za kuchukua dhidi ya Kanda, Kamati au Mwanaumoja aliyekutwa na hatia ya kukiuka taratibu za Umoja;
- (c) Kuushauri Umoja juu ya masuala yanayohusiana na nidhamu;

#### **7.4.2.1.2 Katika kushughulikia masuala ya nidhamu:-**

- (a) Kamati itamwalika mwanaumoja, kumjulisha na kumfafanulia tuhuma dhidi yake;
- (b) Kamati itampa mwanaumoja nafasi ya kujitetea dhidi ya tuhuma zinazomkabili;
- (c) Kamati itachambua utetezi dhidi ya makosa mwanaumoja anayotuhumiwa nayo;
- (d) Kamati ya Nidhamu itaandika uamuzi ambao pande zinazohusika na shauri hilo zitapewa uamuzi; na nakala kwa Katibu wa Kanda anayotoka mlalamikiwa;
- (e) Kamati itatoa uamuzi wa haki, wenye kuzingatia misingi, mila na destuli za utoaji haki ikiwa ni pamoja na kuzingatia sheria za nchi.

#### **7.4.2.1.3 Kamati ya nidhamu na Maadili haitakuwa na mamlaka ya:**

- (a) kushughulikia shauri lolote isipokuwa ambalo limefikishwa mbele yake na Katibu Mkuu; na
- (b) Katibu Mkuu ndiye mlalamikaji katika mashauri yote.

#### **7.4.2.1.4 Kamati ya Nidhamu na Maadili inaweza kuushauri umoja juu ya masuala yahasuyo nidhamu.**

## **Kamati ya Rufaa**

### **7.4.3 Kamati ya Rufaa**

#### **7.4.3.1 Kamati ya Rufaa itapokea, kusikiliza na kutoa uamuzi kwa rufaa zote zitakazopelekwa mbele yake:**

- (a) Na mwanaumoja ambaye hakuridhika na uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili;
- (b) Kwa maandishi akieleza sababu za kutoridhishwa na uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili na nakala kutolewa kwa upande mwingine baada ya kusainiwa na Katibu wa Kamati au mjumbe mwingine na kugongwa mhuri wa Kamati ya Rufaa;
- (c) Ndani ya siku nane bila kujali siku za mwisho wa juma tangu kupokea uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili;

7.4.3.2 Rufaa itapelekwa mbele ya Kamati ya Rufaa iwapo:-

- (a) Kamati ya Nidhamu na Maadili imekiuka masharti ya Katiba na Kanuni katika kutoa uamuzi;
- (b) Uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili umekuwa mkali mno kiasi cha kukiuka misingi ya haki;
- (c) Kamati ya Nidhamu na Maadili haikutoa nafasi ya kujitetea au kusikilizwa;
- (d) Kamati ya Nidhamu na Maadili haikuzingatia utetezi na ushahidi uliotolewa; na
- (e) Kamati ya Nidhamu na Maadili ilisikiliza upande mmoja bila kutoa wito kwa upande mwingine.

7.4.3.3 Kamati ya Rufaa inaweza kupokea rufaa baada ya siku nane kupita tangu mrufani kupokea uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili iwapo kuna sababu za msingi na zenye kuthibitishwa zilizomfanya achelewe kuwasilisha rufaa yake.

## **Kamati ya Fedha na Uchumi**

7.4.4 Kamati ya Fedha na Uchumi

7.4.4.1 Kamati ya Fedha na Uchumi itakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (a) kuibua miradi mbali mbali ya Umoja;
- (b) kutathimini maendeleo ya Umoja kifedha na kiuchumi;
- (c) Kuushauri Umoja juu ya hatua za kuchukua kwa nia ya kujikwamua na kujitegemea kiuchumi;
- (d) kuishauri Kamati Kuu kwa masuala yanayohusu fedha na michango; na
- (e) Majukumu mengine watakayopangiwa na Kamati Kuu, Halmashauri au Mkutano Mkuu

## **Kamati ya Huduma za Jamii**

7.4.5 Kamati ya Huduma za Jamii

7.4.5.1 Kamati ya Huduma za Jamii itakuwa na majukumu yafuatayo:

- (a) Kutoa huduma mbali mbali kwenye matukio ya Umoja
- (b) Kusimamia Ulinzi na Usalama katika matukio mbali mbali ya Umoja
- (c) Kuushauri Umoja namna bora ya utoaji wa huduma; na
- (d) Majukumu mengine watakayopewa na Kamati Kuu, Halmashauri au Mkutano Mkuu.

## **Kamati Maalum**

7.4.6 Kamati Maalum

7.4.6.1 Kamati Maalum inaweza kuundwa na Halmashauri au Mkutano Mkuu baada ya wajumbe wake kupendekezwa na Kamati Kuu.

7.4.6.2 Kamati Maalum:-

- (a) Itaundwa iwapo kuna jambo maalum linalohitaji uchunguzi wa kina;
- (b) Ikiundwa wajumbe wake watatangazwa aidha kwenye Mkutano Mkuu au vikao vya Kanda ili wanaumoja wote wajue.

- (c) kazi za Kamati, hadidu za rejea zitajulikana kwa Wanaumoja wote.
- (d) Mamlaka ya uteuzi ndiyo itakayoamua viongozi wa Kamati maalum.
- (e) taarifa ya matokeo ya kazi itakayofanywa na Kamati husika itawasilishwa kwa mamlaka iliyoiunda.
- (f) Taarifa ya Kamati Maalam itawekwa wazi kwa Wanaumoja wote kupitia ama Mkutano Mkuu au Kanda.
- (g) Uhai na kazi ya Kamati Maalum itaisha baada ya kukabidhi taarifa kwa mamlaka iliyoiunda.

## **Baraza la Wazee na Kamati ya Wazee**

### **7.4.7 Baraza la Wazee**

7.4.7.1 Kutakuwepo na Baraza la wazee. Baraza hili litaundwa na Wanaumoja Wazee wote waliofikisha umri wa miaka 55 au zaidi. Baraza hili litakuwa na jukumu la kuchaugua wajumbe wanne wa Kamati ya Wazee ambayo itafanya kazi kwa niaba ya Baraza. Katika kuchagua wajumbe wa Kamati ya Wazee baraza litazingatia:

- (a) Uwezo wa mzee katika uelewa wa masuala ya Umoja;
- (b) Uwezo wa mzee kuwa mkweli na asiyekuwa mwoga;
- (c) Uwezo wa kuheshimu na kufuata Katiba na Kanuni;
- (d) Uwezo wa kutunza siri za majadiliano na uamuzi; na
- (e) Umakini, kujitoa kwa moyo na jitihada za dhati katika kushughulikia masuala ya Umoja.

7.4.7.2 Kamati ya Wazee itakuwa na majukumu ya:-

- (a) kupokea, kupitia na kuteua wagombea kwa nafasi ya Kamati Kuu; na
- (b) kusuluhisha migogoro ya kiuongozi na kibinafsi kwa viongozi wa Kamati Kuu.

7.4.7.2.1 Katika kusuluhisha migogoro Kamati itazingatia:

- (a) kurudisha maelewano baina ya viongozi;
- (b) ushauri na siyo uamuzi;
- (c) kulinda maslahi mapana ya Umoja; na
- (d) kutoa mawazo huru juu ya kiini cha tatizo;
- (e) kuzisaidia pande zinazohusika kuona ukweli; na
- (f) kutumia busara na ushawishi ili kudhoofisha misimamo kinzani.

7.4.7.2.2 Kamati ya Wazee itashughulikia mgogoro uliofikishwa mbele yake kwa maandishi na:

- (a) Mjumbe yeyote wa Kamati Kuu; au
- (b) Mjumbe yeyote wa Halmashauri.

7.4.7.2.3 Barua ya kupeleka mgogoro mbele ya Kamati ya Wazee sharti:

- (a) leleze kiini kiini cha mgogoro;
- (b) Wahusika katika mgogoro;
- (c) Hatua zilizochukuliwa kuutatua; na
- (d) Taarifa nyingine zinazoweza kuisadia Kamati ya Wazee katika kutatua mgogoro huo.

- 7.4.7.2.4 katika kutekeleza jukumu la usuluhishi, Kamati ya Wazee itawajibika:
- (a) kutafuta taarifa kutoka kwa mtu yeyote juu ya mgogoro unaohitaji usuluhishi;
  - (b) kuwaita na kuongea na viongozi wanoahusika kwenye mgogoro huo; na
  - (c) Mgogoro usipotatuliwa kuandaa taarifa fupi itakayowasilishwa kwenye kikao cha Halmashauri.
- 7.4.7.2.5 kiongozi asipotii wito wa kumtaka afike mbele ya Kamati ya Wazee:-
- (a) Kamati ya Wazee itatoa taarifa ya maandishi kwa Halmashauri;
  - (b) Halmashauri itamhoji kiongozi juu ya sababu za kukaidi wito wa Kamati ya Wazee; na
  - (c) Halmashauri itakapojiridhisha kwamba kiongozi hakuwa na sababu za kutotii wito wa Kamati ya Wazee itachukua hatua zifaazo ikiwa ni pamoja na kupendekeza Mkutano Mkuu umvue uongozi.
- 7.4.7.2.6 Kiongozi atachukuliwa kwamba hakukaidi wito wa Kamati ya Wazee iwapo:
- (a) taarifa ya wito haikumfikia;
  - (b) itathibitika kwamba alishindwa kufika mbele ya Kamati kwa sababu za ugonjwa;
  - (c) Itathibitika kwamba ni kwa sababu ya msiba wa ndugu au jamaa wa karibu naye;
  - (d) Atatoa udhuru kwa sababu ya mwajili wake kumhitaji awe kazini;
  - (e) Itathibitika kwamba alikuwa na wito kwa vyombo vya dola mfano mahakamani au polisi; na
  - (f) Atatoa udhuru wa safari ambayo aliipanga kabla ya kupokea wito wa Kamati ya Wazee.

## **Kamati ya Uchaguzi**

- 7.5 Kutakuwepo na Kamati ya Uchaguzi ambayo itasimamia Uchaguzi Mkuu wa Umoja;
- 7.6 Kamati hii itaongozwa na mwenyekiti atakayechaguliwa na wajumbe wa Kamati;
- 7.7 Wajumbe wa Kamati watamchagua makamu Mwenyekiti wa Kamati Wajumbe wengine watakuwa wajumbe.
- 7.8 Katibu wa Kamati na msaidizi wake watateuliwa na Kamati Kuu miongoni mwa makatibu wa Kanda

## **Kanda**

### 7.9 Kanda Kwenye Muundo wa Umoja

- 7.9.1 Kanda ndicho kitovu na kielelezo cha umoja, undugu na mshikamano wa Wanaumoja wa “Ka nono Group”. Kwa hiyo Kanda siyo kikundi kinachojitegemea kwenye Umoja hivyo:
- (a) Kanda ni sehemu ya Umoja;
  - (b) Kanda haitakuwa na maslahi ambayo yataashiria kutofautiana na Kanda nyingine;
  - (c) Kanda itafanya mambo yaliyoelekezwa na Katiba hii tu;

- (d) Iwapo kanda inataka kuanzisha jambo lolote sharti iombe Kamati Kuu kwa maandishi na Kamati Kuu iridhie kwa maandishi; na
  - (e) Viongozi wa Kanda wanawajibika kusimamia utii wa Katiba na maelekezo ya mamlaka za juu kwenye Umoja.
- 7.9.2 Wanaumoja wasiozidi ishirini (20) au kupungua kumi na watano (15) wanaoishi kwenye eneo linalokaribiana wataunda Kanda moja.
- 7.9.3 Jukumu la kuunda Kanda ni la Kamati Kuu kwa kurejea taarifa za Wanaumoja.
- 7.9.4 Kanda mpya itafanya uchaguzi wa viongozi wake ndani ya siku thelathini tangu kuundwa kwake.
- 7.9.5 Wanaumoja kwenye kanda mpya wataendelea kuwa chini ya kanda mama kwa kipindi ambacho kanda mpya itakuwa haijapata viongozi.
- 7.9.6 Baada ya Kamati Kuu kuunda Kanda, idadi ya wanaumoja kwenye Kanda inaweza kupungua 15 kwa sababu za:
- (a) wanaumoja kuhamia Kanda nyingine;
  - (b) Kufukuzwa kwenye Umoja; na
  - (c) Kufariki;
- 7.9.7 Iwapo wanaumoja kwenye Kanda watapungua na kuwa chini ya wanaumoja kumi (10):-
- (a) Kamati Kuu itarekebisha mipaka ya Kanda jirani ili kuongeza idadi ya wanaumoja kwenye Kanda iliyobaki na wanaumoja chini ya 10; au
  - (b) Itafuta Kanda yenye idadi ndogo ya Wanaumoja na kugawa wanaumoja wa Kanda iliyofutwa kwenye kanda za jirani;
- 7.9.8 Wanaumoja wote lazima wawe chini ya Kanda na waishi ndani ya maeneo ya Kanda walizopangiwa na Kamati Kuu.
- 7.9.9 Kwa utata wowote kuhusu mipaka ya Kanda, Kamati Kuu itawajibika kutoa uamuzi wa kumaliza utata huo na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

### **Kuhama Kanda**

- 7.9.10 Mwanaumoja atakayehamia eneo la Kanda nyingine sharti ajaze fomu ya kuhamia Kanda ya eneo alilohamia. Mwanaumoja ambaye atakiuka masharti ya kifungu hiki:
- (a) Atafikishwa mbele ya Kamati ya Nidhamu na Maadili kwa kosa la kuishi nje ya mipaka ya kanda yake zaidi ya siku thelathini bila kujaza fomu ya kuhama Kanda;
  - (b) Hatapewa huduma yoyote ya Umoja kwa tukio lililomkuta akiishi nje ya mipaka ya Kanda aliyopangiwa zaidi ya siku thelathini ;
  - (c) Katibu Mkuu atawajibika kutoa maelekezo ya kimaandishi kwa Kanda aliyopangiwa ili kumfuta kutoka kwenye orodha ya wanaumoja wa Kanda;
  - (d) Atawajibika kulipa faini ya kutohudhuria vikao vya Kanda; na
  - (e) Atakuwa siyo mwanaumoja hai kuanzia tarehe ya kufutwa kwenye daftari la wanachama wa Kanda aliyopangiwa.

### **Vikao vya Kanda**

- 7.9.11 Wajumbe wa Kanda watakuwa ni wanaumoja wote kwenye Kanda.

- 7.9.12 Kanda zitafanya mikutano kila mwezi isipokuwa miezi ya Septemba, Desemba, Marchi na Juni.
- 7.9.13 Vikao au mikutano ya Kanda itafanyika Jumamosi au Jumapili ya kwanza au ya pili ya mwezi Julai, Agosti, Oktoba, Novemba, Januari, Februari, Aprili na Mei.
- 7.9.14 Kanda inaweza kufanya kikao kimoja cha dharura ndani ya mwezi ambao kuna kikao cha kawaida au mwezi ambao kanda haina kikao cha kawaida.
- 7.9.15 Ili kuwafanya wanaumoya kufahamiana kwa karibu zaidi, mikutano ya kanda lazima ifanyike nyumbani kwa wanaumoya kwa utaratibu wa kila mwanaumoya afikiwe
- 7.9.16 Ili kubakia na Umoja ulio na mshikamano kanda haitakuwa na madai yoyote ambayo ni haki yake lakini si haki kwa kanda nyingine;
- 7.9.17 Mwenyeji wa kikao cha Kanda hawajibiki, ila kwa hiari yake, kuwahudumia wajumbe kwa vinywaji au chakula.
- 7.9.18 Iwapo Mwenyekiti hayupo au amechelewa zaidi ya dakika thelathini wanaumoya wataamchagua mmoja wao kuongoza kikao cha siku hiyo. Wanaumoya hawatamchagua kuongoza kikao cha Kanda:
- (a) Kiongozi wa Kamati Kuu; na
  - (b) Kiongozi wa Kamati ya Kikatiba.
- 7.9.19 Katibu wa Kanda kwa kushirikiana na viongozi wengine watawajibika:
- (a) kutoa taarifa ya wanaumoya waliochelewa kikao cha Kanda zaidi ya dakika 15;
  - (b) kutoa taarifa ya wanaumoya ambao hawakuhudhuria kikao cha Kanda; na
  - (c) kutoa taarifa ya wanaumoya wanaodaiwa ada ya Kanda sawa na miezi mitatu.
- 7.9.20 ili Kamati Kuu kusimamia Kanda ipasavyo:
- (a) Katibu wa Kanda ataandaa na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu ratiba ya mzunguko wa vikao vya Kanda kwa utaratibu wa kila mwanaumoya afikiwe;
  - (b) Katibu wa Kanda ataandaa na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu muhtasari wa kila kikao kinachofanyika kwenye Kanda; na
  - (c) Viongozi wa Kanda wanawajibika kupokea na kuweka wazi kwa wanaumoya taarifa, nyaraka au barua zote watakazopokea kutoka kwa viongozi wa Kamati Kuu.
- 7.9.21 Viongozi wa Kamati Kuu ni wajumbe wa vikao vyote vya Kanda, hivyo kiongozi wa Kamati Kuu yeyote anaweza:-
- (a) Kuhudhuria kikao cha Kanda yoyote bila kuhitaji kutoa taarifa;
  - (b) Kuhesabiwa kwamba amehudhuria kikao cha Kanda hata kama kikao alichohudhuria ni nje ya Kanda aliyopangiwa na Kamati Kuu; na
  - (c) Akiwa kwenye kikao cha Kanda yoyote, isipokuwa Kanda aliyopangiwa na Kamati Kuu, mjumbe wa Kamati Kuu hatapiga kura ya kuamua jambo lolote.

### **Wajibu wa Viongozi wa Kamati Kuu kwenye Vikao vya Kanda**

- 7.9.22 Kwenye vikao vya Kanda, wajumbe wa Kamati Kuu:-
- (a) Watawajibika kutoa miongozo kwa masuala ambayo yanakiuka Katiba;
  - (b) Kusisitiza kanda kuheshimu taratibu na miongozo iliyowahi kutolewa;
  - (c) Kutoa miongozo kwa maamuzi ya Kanda ambayo yanavunja taratibu zilizokubaliwa; na

- (d) Kuhamasisha mahudhurio, michango na undugu miongoni mwa wanaumoja.
- 7.5.23 Vikao vya Kanda ndivyo mamlaka za nidhamu kwa viongozi waliochaguliwa na Kanda. Kanda inaweza:
- (a) Kujadili mwenendo wa Kiongozi wake;
  - (b) Kutoa onyo kwa kiongozi wake;
  - (c) Kumvua uongozi; na
  - (d) Kuomba Kamati Kuu imfikishe Kamati ya Nidhamu endapo anatumuwa kufuja fedha ya mfuko wa Kanda.
- 7.5.24 Katika utekelezaji wa majukumu yake Kanda zitazingatia kuwa:
- (a) zinafanya kazi chini ya uongozi na usimamizi wa Kamati Kuu;
  - (b) zinatawaliwa na Katiba, Kanuni, miongozo na maelekezo ya viongozi wa Kamati Kuu;
  - (c) zinaheshimu mila na desturi ya utawala bora; na
  - (d) zinatambua haki na uwajibikaji.

## Majukumu ya Kanda

- 7.5.25 Kanda itakuwa na majukumu ya msingi yafuatayo:
- (a) Kuwa kiunganishi cha Wanaumoja waliopo kwenye Kanda na wale wa Umoja mkubwa kwa kuhimiza mahudhurio katika vikao, misiba na sherehe za Umoja.
  - (b) Kuhimiza ulipaji wa ada na michango mbali mbali ya Umoja.
  - (c) Kuainisha kero mbali mbali katika Umoja na Wanaumoja hasa kuhusiana na mwenendo wa usimamizi na undeshaji wa masuala ya Umoja
  - (d) Kutafakari juu ya uongozi na maenedeleo ya Umoja ili kama kuna maoni ya kuboresha kuyawasilisha kwa maandishi kwa Katibu Mkuu.
  - (e) Kuibua Wanachama wapya katika kanda na Mkoa wa Arusha kwa ujumla
  - (f) Kuibua mapenedekezo ya kuboresha Katiba ya Umoja
  - (g) Kwa kushirikiana na Kamati Kuu kusimamia nidhamu ya Wanaumoja kwenye Kanda.
  - (h) Kuwa mwenyeji wa msiba unaomhusu mwaumoja kwenye kanda.
  - (i) Kwa kushirikiana na Kamati ya Huduma za Jamii kuratibu shughuli za misiba ya Wanaumoja waliopo kwenye Kanda husika.
  - (j) Kuhimiza Wanaumoja kwenye Kanda, kwa mujibu wa katiba hii, kuhudhuria na kubakia kwenye msiba kwa kushinda na kulala huko hadi msiba utakapomalizika.
  - (k) Kuhakikisha kuwa Wanaumoja waliopo kwenye Kanda hawafanyi jambo lolote linalopingana na katiba, kanuni, maamuzi na maelekezo ya vikao vya Kamati Kuu, Halmashauri, Mkutano Mkuu au viongozi wa wakuu wa Umoja.
  - (l) Kulinda umoja na mshikamano kwa kujizuia na misimamo au matamshi yanayokuza ukanda na utengano kwenye Umoja.

## SURA YA NANE

### Sifa za Viongozi:

- 8.1 Sifa za kiongozi huweza kuwa na tafsiri mbalimbali, lakini kwa malengo ya ibara hii sifa za kiongozi maana yake ni:



- (a) kuzungumza na kujadiliana na watu;
- (b) kueleza, kushawishi na kutoa ushauri unaojenga;
- (c) kufanya kazi kwa vitendo ili kufikia malengo yanayotarajiwa;
- (d) kuchukua wajibu kwa ajili ya Umoja na kutoa mwelekeo; maelekezo na mpangilio;
- (e) kutia moyo watu wengine ili kufikia malengo;
- (f) kuwawezesha wale walio chini yake kutekeleza malengo yaliyowekwa; na

8.2 Kwa hiyo mafanikio ya Umoja yatategemea uongozi bora uliopo, ili aweze kuongoza vizuri, inabidi kiongozi:

- (a) Awe mtu wa kutegemewa katika maamuzi;
- (b) Awe mwenye msimamo (asiyeyumba yumba);
- (c) Awe mwenye uwezo wa kujenga na kusimamia hoja sahihi kwa ujasiri na kwa kujiamini;
- (d) Awe muadilifu katika mwenendo na maisha yake kwa ujumla;
- (e) Awe mwenye kujiamini katika eneo lake la majukumu na mwenye kujitoa kikamilifu katika utendaji;
- (f) Awe mwenye kuweza kufanya maamuzi ndani ya muda, kwa wakati muafaka na kuyasimamia;
- (g) Asiwe mbinafsi, kila wakati ajitoe kwa manufaa ya wengine kabla ya kufikiria atakavyonufaika yeye;
- (h) Asitumie nafasi yake kwa faida yake, watu alio na nasaba nao au uswahiba;
- (i) Awe msemwa kweli daima na fitina kwake iwe ni mwiko;
- (j) Awe ni mtu mwenye maarifa na ujuzi;
- (k) Awe mwenye moyo wa kusamehe, asiwe mlipa visasi;
- (l) Asiwe na matumizi mabaya ya rasilimali zilizopo;
- (m) Awe ni mtu jasiri katika kukabiliana na changamoto za taasisi;
- (n) Awe mbunifu, muwazi, mkweli na muadilifu;
- (o) Awe na uelewa kuhusu kanuni, sera, katiba dira na dhima ya Umoja;
- (p) Awe mpashanaji habari mzuri kwa kutumia mikondo rasmi ya mawasiliano;
- (q) Awe anajua jinsi ya kushughulikia mizozo, migongano na migogoro;
- (r) Atambue kwamba binadamu hutofautiana katika sifa na uwezo wa kufikiri, utashi, hulka, tabia na imani;
- (s) Awe na uwezo wa kuwaunganisha wanaumoja katika kutekeleza mambo yanayowahusu; na

### **Kipimo cha Uongozi wa Umoja**

8.3 Katika kutekeleza majukumu yake, uongozi utapimwa kwa sifa zifuatazo:

- (a) kusimamia utelekezaji wa katiba, kanuni na maamuzi ya vikao;
- (b) kuwa wahamasishaji na waelimishaji wa wale wanaowangoza ili kujenga umoja unaoheshimu taratibu na miongozo iliyopo;
- (c) kubuni na kuweka mipango mahsusi inayotuelekeza kwenye malengo ya Umoja;
- (d) kubuni mbinu mbalimbali za kutunisha mfuko ili kufanikisha utoaji wa huduma;

- (e) kuratibu shughuli zote za Umoja kwa kusimamia kwa karibu kanda na kamati za kikatiba;
- (f) kutoa miongozo mbalimbali kwa viongozi wa Kanda ili uendeshaji wa Kanda usitofautiane kati ya kanda moja na nyingine;
- (g) kutatua matatizo yanayojitokeza kwenye kanda ili kuzifanya ziwe imara;
- (h) kudhibiti uvunjifu wa taratibu ili kuimarisha nidhamu na utii kwa taratibu zilizokubaliwa;
- (i) kupiga vita ubaguzi na matabaka kwa misingi ya ukabila au hali ya kijamii;
- (j) kupokea na kushughulikia malalamiko ya wanaumoja;
- (k) kutafuta fursa mbalimbali ambazo wanaumoja wanaweza kufaidika nazo;
- (l) kuhimiza maendeleo ya wanaumoja; na
- (m) kuhimiza umoja na mshikamano wa wanaumoja wote.

### **Masharti ya kuwa Kiongozi kwenye Umoja**

8.4 Ili Mwanaumoja aweze kuwa kiongozi sharti:

- (a) Awe ametimiza angalau mwaka mmoja tangu kujiunga na Umoja;
- (b) Awe hajatumikia zaidi ya vipindi viwili vya uongozi kwa nafasi ileile;
- (c) Kama amestaafu baada ya kutumikia vipindi viwili vya miaka mitatu kila kimoja, awe amepumzika kwa angalau kipindi kimoja cha miaka mitatu.

## **SURA YA TISA**

### **Uchaguzi wa Viongozi**

9 Uchaguzi wa Viongozi kwenye Umoja

9.1 Mkutano Mkuu wa Uchaguzi

- 9.1.1 Mkutano Mkuu wa uchaguzi utaitishwa Jumapili ya tatu ya mwezi August.
- 9.1.2 Iwapo kuna sababu za msingi, mkutano mkuu wa uchaguzi unaweza kuitishwa Jumapili ya pili ya Mwezi August lakini kwa vyovyote vile isiwe zaidi ya Jumapili ya nne ya Mwezi August.
- 9.1.3 Mkutano Mkuu wa uchaguzi utaitishwa na Katibu Mkuu baada ya kushauriana na Mwenyekiti.
- 9.1.4 Mwenyekiti atafungua Mkutano Mkuu wa uchaguzi na kuwakaribisha wajumbe wa Kamati ya Uchaguzi wachukue nafasi yao.

### **Viongozi kujiuzulu**

- 9.1.5 Baada ya wajumbe wa kamati ya uchaguzi kujongea mbele, Mwenyekiti wa Umoja atatangaza kujiuzulu na hivyo kumaliza muda wa uongozi wake na viongozi wengine;
- 9.1.6 Viongozi ambao kwa tangazo la mwenyekiti la kujiuzulu uongozi wao utakuwa umekoma ni:
  - (a) Mwenyekiti;
  - (b) Makamu Mwenyekiti;

- (c) Katibu Mkuu;
  - (d) Katibu Mkuu Msaidizi;
  - (e) Mweka Hazina;
  - (f) Mweka Hazina Msaidizi; na
  - (g) Wajumbe wa Kamati za Kikatiba.
- 9.1.7 Viongozi waliomaliza muda wao wa uongozi wataondoka meza kuu na Kamati ya Uchaguzi itachukua nafasi ili kusimamia uchaguzi.
- 9.1.8 Mchakato wa kuwapata viongozi utanza mwezi Julai kwa Kanda kufanya vikao vya kupendekeza wagombea wa nafasi za viongozi wa Kamati Kuu.

### **Upatikanaji wa Viongozi: Mchakato kwenye Kanda**

- 9.1.9 Kila kanda itapendekeza jina la mgombea kwa nafasi ya:
- (a) Mwenyekiti
  - (b) Katibu Mkuu
  - (c) Mweka Hazina
- 9.1.10 Iwapo kanda itamuona anafaa, inaweza kumpendekeza mgombea kutoka kanda nyingine.
- 9.1.11 Katika kupendekeza majina Kanda:-
- (a) Haitapendekeza mwanaumwa ambaye hajamaliza mwaka mmoja tangu ajiunge na Umoja;
  - (b) Haitapendekeza mwanaumwa ambaye ametumikia vipindi viwili vya uongozi;
  - (c) Haitapendekeza mwanaumwa aliyefukuzwa uongozi au aliyeshinikizwa kujiuzulu kwa makosa aliyoyatenda akiwa kiongozi;
  - (d) Haitapendekeza mwanaumwa ambaye hajui kusoma na kuandika;
  - (e) Haitapendekeza Mwanaumwa anayeishi nje ya Halmashauri ya Meru, Jiji na Halmashauri ya Arusha; na
  - (f) Haitapendekeza mwanaumwa ambaye siyo hai.
- 9.1.12 Makatibu wa Kanda watakabidhi kwa Katibu Mkuu Majina ya Wanaumwa iliyowapendekeza.

### **Kukabidhi Majina Kamati ya Wazee**

- 9.1.13 Baada ya kupokea majina ya wanaumwa waliopendekezwa na kanda kugombea uongozi, ndani ya siku zisizozidi saba Katibu Mkuu atawajibika:
- (a) Kutengeneza orodha ya wagombea kwa utaratibu unaofaa;
  - (b) Kutuma kwenye Kanda majina ya wagombea wote waliopendekezwa;
  - (c) Kuandika barua ya kuwasilisha (covering letter) majina ya wagombea kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wazee; na
  - (d) Kuwasilisha na kukabidhi majina ya wagombea kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wazee.
- 9.1.14 Mapema iwezekanavyo na kabla ya Kamati ya wazee kufanya kikao cha kujadili na kupitisha wagombea kwa kila nafasi:

- (a) Mgombea yeyote aliyependekezwa na Kanda tofauti na Kanda yake anaweza kumwandikia Mwenyekiti wa Kamati ya Wazee kumweleza sababu za msingi ambazo zitamfanya ashindwe kutumikia Umoja iwapo atachaguliwa; na
  - (b) Mgombea ambaye wakati anapendekezwa na Kanda yake kugombea uongozi hakuwa amejua sababu ambazo zitamfanya ashindwe kutumikia umoja endapo atachaguliwa atamwandikia Mwenyekiti wa Kamati ya Wazee kumweleza.
- 9.1.15 Mwenyekiti wa Kamati ya Wazee atahifadhi mahala pa usalama majina ya wanaumoja kama alivyoyapokea kutoka kwa Katibu Mkuu mpaka:
- (a) Atakaposhauriana na kukubaliana na Katibu wa Kamati kuitisha kikao cha uteuzi wa mwisho wa wagombea;
  - (b) Kikao cha Kamati ya Wazee cha uteuzi wa wagombea kitakaa ndani ya siku saba kabla ya uchaguzi na kuchuja majina ya wagombea;
  - (c) Akidi ya kikao itakuwa asilimia 50
  - (d) Ili kuzuia kampeni, majina ya wagombea waliopitishwa kwa kila nafasi na wale walioachwa yatabaki siri ya Kamati ya Wazee mpaka mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi atakapofungua bahasha na kusoma majina ya wagombea waliopitishwa.

### Kuteua Wagombea wa Uongozi

- 9.1.16 Kutoka kwenye majina yaliyopendekezwa na Kanda, Kamati ya Wazee itapitisha wagombea wawili au watatu kwa kila nafasi ya:
- (a) Mwenyekiti;
  - (b) Makamu Mwenyekiti;
  - (c) Katibu Mkuu;
  - (d) Katibu Mkuu Msaidizi;
  - (e) Mweka Hazina; na
  - (f) Mweka Hazina Msaidizi.
- 9.1.17 Katika kuchambua, kujadili na kupitisha majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi wajumbe wa kamati ya wazee wanawajibika:
- (a) Kuzingatia maslahi mapana ya Umoja;
  - (b) Kuzingatia uwezo wa kila mgombea katika kutumikia nafasi ambayo amependekezwa; na
  - (c) Kutunza siri za majadiliano na uamuzi ili kuzuia uwezekano wa kampeni; na
  - (d) Kuzingatia sababu zilizoainishwa na wagombea ambao wameandika barua kueleza sababu ambazo zitawafanya washindwe kutumikia Umoja iwapo watachaguliwa.
- 9.1.18 Kamati ya wazee katika kujadili na kuteua wagombea wa uongozi wa Umoja inakatazwa kujihusisha na:-
- (a) ushabiki, ubaguzi wa kijinsia au ubaguzi mwingine wa moja kwa moja au usiokuwa wa moja kwa moja;
  - (b) ushawishi wa viongozi au mtu yeyote ambaye siyo mjumbe wa Kamati;

- (c) maslahi binafsi, undugu, ukanda au nasaba;
  - (d) mitazamo ya kisiasa, mugegemeo wa imani za kidini na hali ya mtu kijamii; na
  - (e) ubaguzi kwa misingi ya eneo analotoka mgombea.
- 9.1.19 Majina ya wagombea waliopitishwa kwa kila nafasi yatawekwa kwenye bahasha ambayo:
- (a) Itafungwa ipasavyo
  - (b) Juu yake itaandikwa nafasi ambayo wagombea wamepitishwa kugombea
  - (c) Itakabidhiwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi baada ya kugawa karatasi za kura lakini kabla ya kupiga kura kwa nafasi husika.
- 9.1.20 Kamati ya Uchaguzi haitagawa karatasi za kupiga kura mpaka:
- (a) Wageni na wanaumoja wasiokuwa hai wametengewa nafasi maalum ili wasipige kura;
  - (b) Wanaumoja ambao hawajatimiza mwaka mmoja tangu wajiunge wametambuliwa na kutambulishwa kwa wapiga kura ili wasichaguliwe;
  - (c) Wanaumoja wenye sifa za kupiga kura wamehesabiwa ipasavyo; na
  - (d) Wapiga kura waliohudhuria siyo chini ya asilimia 60% ya Wanaumoja wote kwa mujibu wa taratibu za upigaji kura.
- 9.1.21 Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi hatafungua bahasha yenye majina ya wagombea kwa nafasi husika mpaka:
- (a) Ajiridhishe kwamba bahasha inayofunguliwa imeandikwa juu yake nafasi inayogombewa;
  - (b) Karatasi za kupiga kura zimegawiwa ipasavyo kwa wapiga kura;
  - (c) Amejiridhisha kwamba hakuna mazingira ya kupiga kampeni kabla na baada ya kutangaza wagombea;
  - (d) Amejiridhisha kwamba wapiga kura wapo tayari kupiga kura; na
  - (e) Baada ya kujiridhisha Mwenyekiti wa Kamati ya uchaguzi atafungua bahasha, kuwasoma majina na kuwatangaza wagombea wa nafasi ambayo wapiga kura wametayarishwa kuchagua.
- 9.1.22 Viongozi watachaguliwa kwa mtiririko ufuatao:
- (a) Mwenyekiti
  - (b) Makamu Mwenyekiti
  - (c) Katibu Mkuu
  - (d) Katibu Mkuu Msaidizi
  - (e) Mweka Hazina;
  - (f) Mweka Hazina Msaidizi; na
  - (g) Wajumbe wa Kamati za Kikatiba.

### **Utaratibu wa Kuwachagua Wajumbe wa Kamati za Kikatiba**

- 9.1.23 Wajumbe wa Kamati ya Nidhamu na Maadili, Kamati ya Huduma za Jamii na Kamati ya Fedha na Uchumi watachaguliwa na Wanaumoja kwenye Mkutano Mkuu wa

uchaguzi kwa kupigiwa kura za papo hapo kutoka miongoni mwa wanaumoj ambao wametimiza angalau mwaka mmoja tangu kujiunga.

- 9.1.24 Wapiga kura watachagua;
- (a) Wajumbe wanne wa Kamati ya Nidhamu na Maadili;
  - (b) Wajumbe saba wa Kamati ya Huduma za Jamii; na
  - (c) Wajumbe wanne wa Kamati ya Fedha na Uchumi.
- 9.1.25 Wagombea watakaopata kura nyingi ndiyo watakaokuwa wamechaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati za kikatiba.
- 9.1.26 Baraza la Wazee litachagua wajumbe watano wa Kamati ya Wazee.
- 9.1.27 Kiongozi akishachaguliwa kwenye nafasi ya juu asichaguliwe kwenye nafasi ya chini. Ngazi za uongozi zinafuatana kama ifuatavyo:
- (a) Mwenyekiti;
  - (b) Makamu Mwenyekiti;
  - (c) Katibu Mkuu;
  - (d) Katibu Mkuu Msaidizi;
  - (e) Mweka Hazina;
  - (f) Mwekea Hazina Msaidizi;
  - (g) Wenyeviti wa Kamati za Kikatiba;
  - (h) Makatibu wa Kamati za Kikatiba;
  - (i) Weka Hazina wa Kamati za Kikatiba;
  - (j) Wajumbe wa Kamati za Kikatiba;
  - (k) Wenyeviti wa Kanda;
  - (l) Makatibu wa Kanda; na
  - (m) Weka Hazina wa Kanda.

### **Uchaguzi wa Viongozi wa Kanda na Kamati za Kikatiba**

- 9.1.28 Viongozi wa Kamati za Kikatiba watachaguliwa ndani ya siku 30 tangu uchaguzi mkuu kufanyika:
- (a) Kwa wajumbe wa Kamati kumchagua Mwenyekiti wa Kamati
  - (b) Kwa wajumbe wa Kamati kumchagua Mweka Hazina wa Kamati
  - (c) Baada ya kushauriana na kukubaliana na Mwenyekiti, lakini kabla ya uchaguzi wa viongozi wa kamati, Katibu Mkuu atawateua makatibu wa Kamati za Kikatiba kutoka miongoni mwa wanaumoj ambao ni hai na wametimiza mwaka mmoja tangu kujiunga na Umoja.

### **Wasimamizi wa Uchaguzi kwenye Kanda na Kamati za Kikatiba**

- 9.1.29 Viongozi wa Kamati Kuu au viongozi wengine watakaoteuliwa na Kamati Kuu watasimamia uchaguzi wa viongozi wa Kamati za kikatiba na uchaguzi wa viongozi wa Kanda.

### **Utaratibu wa Uchaguzi kwenye Kanda**

- 9.1.30 Uchaguzi wa Kanda utafuata utaratibu ufuatao:

- (a) Akidi ya Mkutano wa uchaguzi wa Kanda itakuwa ni wajumbe wasiopungua asilimia 75 ya wapiga kura wote kwenye kanda;
- (b) Kila mwanaumoja kwenye Kanda ni mgombea wa uongozi wa kanda;
- (c) Wajumbe wa mkutano wa uchaguzi wa kanda watapiga kura za siri;
- (d) Kura za papo kwa papo zitapigwa na atakayepata kura nyingi, lakini siyo chini ya asilimia 50 ya kura zilizopigwa, ndiye atakayekuwa amechaguliwa;
- (e) Wapigakura kwenye Kanda watachagua Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina;
- (f) Mshindi wa nafasi ya uenyekiti atatangazwa kabla ya kuchagua Mweka Hazina wa Kanda;
- (g) Viongozi wa Kanda wataanza kutekeleza majukumu ya uongozi mara tu baada ya kusimikwa rasmi.

## **Kuwasimika Viongozi**

9.1.31 Kusimika Viongozi;

- (a) Mshindi wa nafasi ya uongozi atatangazwa kabla ya kuchagua kiongozi anayefuata;
- (b) Uchaguzi ukisha kamilika mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi atawaalika viongozi wateule kujongea mbele;
- (c) Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi atawaalika wanaumoja kuwashangilia viongozi wateule;
- (d) Kuwashangilia viongozi ni kuashiria kwamba viongozi wateule sasa wamesimikwa rasmi;
- (e) Utaratibu uliotajwa kwenye (a) – (d) utatumika kuwasimika viongozi kwenye Kanda, Kamati za Kikatiba na Mkutano Kuu.

## **Masuala yanayoweza kumfanya Mwanaumoja asichaguliwe kuwa kiongozi**

9.1.32 Mwanaumoja hatachaguliwa kwenye nafasi ya uongozi iwapo:

- (a) nafasi anayotegemea kuchaguliwa ni ya chini ikilinganishwa na nafasi aliyokuwa akitumikia;
- (b) siyo mwanaumoja hai;
- (c) hajakaa kwenye Umoja kwa mwaka mmoja au zaidi tangu kujiunga;
- (d) anaishi kwenye eneo la mbali au kwa sababu nyingine linamfanya ashindwe kupatikana kwa urahisi; na

## **SURA YA KUMI**

### **Majukumu ya Viongozi**

10 Majukumu ya Viongozi

10.1 Viongozi wa Umoja katika utekelezaji wa kazi zao za kila siku watakuwa na majukumu yafuatayo:-

10.1.1 Mwenyekiti;

- (a) Kiongozi mkuu na msingi wa Umoja ambaye atasimamia na kuangalia shughuli zote za Umoja;
- (b) Kutoa falsafa na mwelekeo wa kiuongozi kwa viongozi wengine;
- (c) Kusimamia na kuelekeza viongozi wanaomsaidia kuongoza Umoja;
- (d) Kusimamia na kuhimiza ukuu wa katiba na utii wa Katiba kwa viongozi ngazi zote na wanaumoja wote;
- (e) Ni mlezi na mlinzi wa Umoja;
- (f) Kuendesha na kusimamia Vikao vyote vya Mkutano Mkuu, Halmashauri, na Kamati Kuu;
- (g) Msimamizi mkuu wa nidhamu ndani na nje ya vikao vya Umoja;
- (h) Pamoja na Katibu Mkuu kutia saini katika kumbukumbu za mikutano ya Umoja;
- (i) Kupiga kura ya turufu kama kura zitafungana katika maamuzi; na
- (j) Kuwakilisha Umoja katika mialiko na shughuli mbalimbali.

10.1.2 Makamu Mwenyekiti ni Msaidizi wa Mwenyekiti na ambaye atafanya kazi zote za Mwenyekiti kama:-

- (a) Mwenyekiti hayupo au wakati Mwenyekiti amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kuugua, kusafiri au sababu nyingine zenye kufanana na hizo; na
- (b) Mwenyekiti amejiuzulu au kufukuzwa uongozi.

10.1.3 Katibu Mkuu atakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (a) Mtendaji na mratibu Mkuu wa shughuli za Umoja;
- (b) Mtekelezaji Mkuu wa maamuzi ya vikao vya Mkutano Mkuu, Halmashauri na Kamati Kuu;
- (c) Kuitisha vikao vya Umoja baada ya kushauriana na Mwenyekiti;
- (d) Kuandika na kusoma mihtasari ya vikao;
- (e) Kuweka kumbukumbu zote za Umoja;
- (f) Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya vikao vya Umoja;
- (g) Kubuni miongozo ya uendeshaji bora wa Kanda;
- (h) Kwa kushirikiana na viongozi wa Kanda kuratibu uendeshaji bora wa Kanda;
- (i) Kwa kushirikiana na viongozi wa Kamati za Kikatiba kuratibu uendeshaji bora wa Kamati za kikatiba;
- (j) Kiunganishi cha shughuli za Umoja ngazi ya Kanda, Kamati na Umoja kwa ujumla; na  
Pamoja na Mwenyekiti kutia saini katika kumbukumbu za mikutano yote ya Umoja.

10.1.4 Katibu Mkuu Msaidizi ni Msaidizi wa Katibu Mkuu ambaye atafanya kazi zote za Katibu Mkuu kama Katibu Mkuu hayupo au kazi atakazoelekezwa kufanya na Katibu Mkuu au mamlaka nyingine.

10.1.5 Mweka Hazina atakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (a) Kupokea na kutunza fedha na mali za Umoja;
- (b) kuandaa, kuhakiki na kutoa taarifa za fedha zinazohusu ada, viingilio na



michango mingine ya Wanaumoja;

- (c) Kuandaa taarifa za mapato, matumizi na madeni ya Wanaumoja kila mwezi;
- (d) Kuwasilisha Taarifa zote za fedha Kamati Kuu, Halmashauri na Mkutano Mkuu;
- (e) Kutoa nakala za taarifa ya fedha kwenye Kanda ili kila Mwanaumoja anayetaka kupata nakala ya taarifa hiyo aipate kwa urahisi;
- (f) Kufanya malipo mbalimbali na kutunza nakala za stakabadhi;
- (g) Kutoa stakabadhi kwa fedha iliyopokelewa na Umoja;
- (h) Kuboresha taratibu za ulipaji wa fedha kwa Wanaumoja kwa huduma zilizoainishwa ili kusiwepo na usumbufu wala ucheleweshaji wa huduma;
- (i) Kuboresha na kusimamia taratibu za kutoa mikopo na marejesho yake; na
- (j) Bila kuathiri masharti ya Katiba hii kuidhinisha kiasi cha mchango utakaotzwa na kanda kama ada ya Kanda.

10.1.6 Mweka Hazina Msaidizi ni Msaidizi wa Mweka Hazina ambaye atafanya kazi zote za Mweka Hazina kama hayupo na kazi nyinginezo kwa maelekezo ya Mweka Hazina au mamlaka nyingine.

10.1.7 Mwenyekiti wa Kamati atakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (a) Kiongozi mkuu na msingi wa Umoja ambaye atasimamia na kuelekeza shughuli zote za Umoja ngazi ya Kamati;
- (b) Kuendesha na kusimamia Vikao vyote vya kamati. Mwenyekiti asipokuwepo, wajumbe watamchagua mmoja wao kuongoza kikao;
- (c) Msimamizi mkuu wa nidhamu katika vikao vya Umoja ngazi ya kamati kwa mujibu wa Katiba hii;
- (d) Pamoja na Katibu wa Kamati kutia saina katika kumbukumbu za mikutano yote ya Umoja ngazi ya kamati;
- (e) Kupiga kura ya turufu kama kura zitalingana katika maamuzi; na
- (f) Kuwakilisha Umoja ngazi ya kamati katika mialiko na shughuli mbalimbali

10.1.8 Katibu wa Kamati atakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (a) Mtendaji na mratibu Mkuu wa shughuli za Umoja kwenye kamati;
- (b) Kuitisha vikao vya Kamati husika baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa kamati;
- (c) Kuandika na kusoma mihtasari ya vikao vya kamati;
- (d) Kuweka kumbukumbu zote za Umoja ngazi ya kamati;
- (e) Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya vikao vya juu vya Umoja na vya kamati yake; na
- (f) Pamoja na Mwenyekiti kutia saina katika kumbukumbu za mikutano yote ya Umoja ngazi ya kamati.

10.1.9 Mweka Hazina wa Kamati atakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (a) Kuandaa bajeti ya kamati na kuiwasilisha kwa mweka Hazina Mkuu;
- (b) Kuwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa Mweka hazina mkuu;

- (c) Kufanya malipo mbalimbali na kutunza nakala za stakabadhi; na
- (d) Ni katibu msaidizi wa kamati.

10.1.10 Mwenyekiti wa Kanda atakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (a) Kiongozi mkuu na msingi wa Umoja ambaye atasimamia na kuelekeza shughuli zote za Umoja ngazi ya kanda;
- (b) Mwakilisha wa Kanda kwenye Halmashauri na kutoa mrejesho wa vikao vya Halmashauri kwenye vikao vya Kanda zao;
- (c) Msimamizi mkuu wa utekelezaji na utii wa Katiba ya Umoja ngazi ya Kanda;
- (d) Kuendesha na kusimamia Vikao vyote vya kanda;
- (e) Mpokeaji na msimaizi mkuu wa utekelezaji wa maelekezo ya vikao vya Kamati za Kikatiba, Kamati Kuu, Halmashauri, Mkutano Mkuu na maelekezo kutoka kwa viongozi wa juu;
- (f) Msimamizi mkuu wa nidhamu katika vikao vya Umoja ngazi ya kanda kwa mujibu wa Katiba hii;
- (g) Pamoja na Katibu wa Kanda kutia saina katika kumbukumbu za mikutano yote ya Umoja ngazi ya kanda;
- (h) Kupiga kura ya turufu kama kura zitalingana katika maamuzi;
- (i) Kuwakilisha Umoja ngazi ya kanda katika mialiko na shughuli mbalimbali;
- (j) Mwenyekiti asipokuwepo, wajumbe watamchagua mmoja wao kuongoza kikao hicho; na
- (k) Mjumbe wa kikao cha Halmashauri.

10.1.11 Katibu wa Kanda atakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (a) Mtendaji na mratibu Mkuu wa shughuli za Umoja ngazi ya kanda;
- (b) Kuitisha vikao vya Umoja baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa kanda;
- (c) Kuandika, kuhifadhi na kusoma mihtasari ya vikao vya Kanda;
- (d) Kuweka kumbukumbu na nyaraka zote za Umoja ngazi ya kanda;
- (e) Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya vikao vya juu vya Umoja na vya kanda yake;
- (f) Kutekeleza maelekezo ya mwenyekiti wa Kanda na viongozi wa Kamati Kuu;
- (g)** Pamoja na Mwenyekiti kutia saina katika kumbukumbu za mikutano yote ya Umoja ngazi ya kanda.

10.1.12 Mweka Hazina wa Kanda atakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (a) Kupokea na kuweka ada ya Wanaumoja ngazi ya kanda;
- (b) Kuandaa taarifa ya mapato, matumizi na madeni ya Wanaumoja kila mwezi;
- (c) Kuwasilisha, kusoma na kuweka wazi taarifa zote za fedha kwenye mkutano wa kanda;
- (d) Kutafuta na kutunza nakala za taarifa za fedha za Umoja ili kila Mwanaumoja anayetaka kupata nakala ya taarifa hizo azipate kwa urahisi na kwa gharama zake;
- (e) Kusimamia taratibu za ukusanyaji wa ada ya kanda;

- (f) Kukusanya kutoka kwa wanaumoja mchango wa Kanono Day; na
- (g) Ni katibu msaidizi wa kanda.

## SURA YA KUMI NA MOJA

### Uwajibikaji wa Viongozi

#### 11 Uwajibikaji wa Viongozi wa Umoja

- 11.1 Ili kuleta ustawi endelevu kwenye Umoja viongozi wa Umoja ngazi zote wanawajibika kuheshimu Katiba, Kanuni, maamuzi ya vikao na miongozo mbalimbali.
- 11.2 Katika kutekeleza majukumu ya kila siku, kila kiongozi anawajibika:
  - (a) Kutumia raslimali za Umoja kwa uadilifu wa hali ya juu ili ziwanufaishe wanaumoja bila ubaguzi au upendeleo katika utoaji wa huduma;
  - (b) Kila kiongozi azingatie ukuzwaji wa uwazi, ushirikishwaji na uwajibikaji wa kila mwanaumoja katika kuheshimu, kufuata na kulinda taratibu za Umoja;
  - (c) Viongozi wachunge na kuangalia vitendo vyao na wawajibike kwa maslahi mapana ya Umoja;
  - (d) Kila kiongozi anawajibika kusimamia taratibu za Umoja kwa kujenga uelewa kwa wanaumoja na kutafuta miongozo kutoka viongozi wa ngazi za juu au vikao;
  - (e) Kiongozi anawajibika kuelimisha, kukemea na kuonya juu ya matendo yanayokiuka katiba moja kwa moja au kwa namna ambayo yanajenga mitazamo au mazoea ambayo baadaye yatazalisha tabia zitakazokinzana na Katiba au ustawi wa Umoja;
  - (f) Kila kiongozi atahakikisha kwamba uendeshaji wa shughuli za Umoja kwenye Kanda hazitofautiani kati ya Kanda moja na nyingine; na
  - (g) Viongozi wahudhurie vikao vya Kanda na vikao vinavyowahusu kwa asili ya nafasi zao.
- 11.3 Uwajibikaji wa kiongozi utapimwa katika mambo yafuatayo:
  - (a) Utekelezaji wa majukumu yake na kwa wakati;
  - (b) Kuamini katika ukuu wa katiba kama muongozo mkuu wa uendeshaji wa shughuli zote za Umoja;
  - (c) Kusimamia ukuu na utii wa katiba katika Umoja;
  - (d) Kutoa muda wake kufanya shughuli za Umoja bila manung'uniko yanayoweza kuathiri uendeshaji wa Umoja;
  - (e) Kutambua kwamba kiongozi anawajibika kwa matendo na maamuzi yake;
  - (f) Kujiepusha kuchochoea wanaumoja kupingana na maamuzi halali ya kiongozi, kikao, mkutano, kanuni au katiba; na
  - (g) Kiongozi anawajibika kwanza kwa Katiba ya Umoja.
- 11.4 Kiongozi anayekiuka misingi ya uwajibikaji:
  - (a) Mwanaumoja au kiongozi yeyote atamkumbusha kurudi kwenye misingi ya katiba, kanuni na taratibu za Umoja;

- (b) Kama kiongozi aliyekiuka misingi ya Katiba ni kiongozi wa Kanda au Kamati ya kikatiba, Kamati Kuu itamjadili na ikimkuta na kosa la kukiuka katiba, inaweza kumwandikia barua ya onyo; na
  - (c) Kama kiongozi aliyekiuka misingi ya Katiba ni kiongozi wa Kamati Kuu, Halmashauri inaweza kumjadili na kumuandikia barua ya onyo.
- 11.5 Mwanaumoja yeyote atawasilisha kwenye Kanda, Kamati Kuu, Halmashauri au Mkutano Mkuu hoja ya Kiongozi kujiuzulu iwapo moja au zaidi ya yafuatayo litatokea:
- (a) Iwapo kiongozi atathibitika kufuja fedha za Umoja;
  - (b) Iwapo kiongozi atathibitika kupokea fedha taslim kutoka kwa Mwanaumoja kinyume na maelekezo ya Katiba;
  - (c) Iwapo kiongozi atapokea fedha taslim kutoka kwa mtu anayetaka kujiunga na Umoja;
  - (d) Iwapo atashindwa kuhudhuria mfululizo vikao vitatu vya kikao ambacho yeye ni mjumbe bila sababu za msingi;
  - (e) Endapo atashindwa kulipa ada ya Umoja kwa miezi mitano; na
  - (f) Endapo atafungiwa huduma kwa kosa la kudaiwa harambee, mchango wa kutunisha, adhabu au mchango wowote.
- 11.6 Kiongozi atajwajibika kujiuzulu mwenyewe au asipojiuzulu kwa hiari kusababisha ajiuzulu iwapo:
- (a) atachaguliwa kwenye nafasi ambayo ametumikia kwa vipindi viwili mfululizo;
  - (b) anahamia maeneo ambayo hawezi kutimiza wajibu wake kama kiongozi; na
  - (c) atachaguliwa akiwa hajamaliza mwaka mmoja tangu kujiunga na Umoja.

## SURA YA KUMI NA MBILI

### Marekebisho ya Katiba

#### 12 Marekebisho ya Katiba ya Umoja

- 12.1 Mabadiliko ya Katiba yatafanyika kila baada ya miaka mitano.
- 12.2 Kamati Kuu itaunda Kamati ya Katiba mwezi April au kabla na kuwasilisha majina ya wajumbe kwenye Halmashauri ya Umoja ambayo:
  - (a) Inaweza kubadilisha muundo, idadi na aina ya wajumbe wa Kamati ya katiba iwapo kuna sababu za msingi; na
  - (b) Itaridhia iwapo hakuna sababu za msingi za kufanya mabadiliko.
- 12.3 Kamati ya Katiba itanza kazi rasmi mara baada ya kuridhiwa na Halmashauri;
- 12.4 Kamati ya Katiba itakamilisha kazi ya kuandika rasimu ya katiba mwezi Juni na katiba itapitishwa na Mkutano Mkuu mwezi Julai;
- 12.5 Maoni ya marekebisho ya Katiba yatakusanywa kwa utaratibu ufuatao-
  - (a) Mwanaumoja atawasilisha kwa katibu wa Kanda yake maoni ya marekebisho ya katiba kwa maandishi muda wowote anapogundua mapungufu kwenye katiba inayotumika;
  - (b) Katibu wa kanda ataweka maoni ya mwanaumoja mahala pa usalama;
  - (c) Katibu wa Kanda atawasilisha maoni hayo kwa Kamati ya Marekebisho ya Katiba muda wa kurekebisha Katiba utakapowadia; na

- (d) Mwanaumojia atafuatilia kuhakikisha kwamba Kamati ya Kurekebisha Katiba imepokea maoni yake; na
  - (e) Kamati ya Katiba itaweka utaratibu muafaka kwa ajili ya kupata maoni kutoka kwa wanaumojia wengi kadri iwezekanavyo.
- 12.6 Iwapo kwa sababu zozote zile idadi ya wajumbe wa Kamati ya Katiba itapungua-
- (a) Kamati Kuu itaongeza wajumbe kulingana na idadi ya wajumbe waliopungua;
  - (b) Kama hakuna kikao cha Kamati Kuu kinachotarajia kuitishwa ndani ya siku 15 tangu idadi ya wajumbe kupungua, Katibu Mkuu baada ya kushauriana na Mwenyekiti atateua wajumbe kujaza nafasi zilizoachwa wazi.
- 12.7 Katika marekebisha ya katiba Kamati inashauriwa kuwa na mashauriano yatakayosaidia kufikia makubaliano kwa muafaka na maelewano. Iwapo hili halitawezekana:
- (a) Makubaliano yatafikiwa kwa njia ya kupiga kura; na
  - (b) Iwapo kura zitagawanyika nusu kwa nusu mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.
- 12.8 Katika kupitisha vifungu vya katiba na hatimaye katiba nzima, vifungu ambavyo vitazua mabishano-
- (a) Wanaumojia watazingatia maelezo ya wajumbe wa Katiba;
  - (b) Iwapo kuna haja kura zitapigwa na kifungu kitapitishwa kwa kura za wanaumojia wengi; na
  - (c) Kama kura zitalingana Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.
- 12.9 Baada ya kupitisha kifungu cha mwisho wanaumojia watapiga kura kupitisha katiba nzima.
- 12.10 Baada ya Katiba nzima kuipitisha-
- (a) Kamati ya marekebisha ya katiba itaingiza nyongeza ya vifungu vilivyoamuliwa na Mkutano Mkuu; na
  - (b) Isipokuwa makosa ya kiuchapishaji tu, kamati ya katiba haitafanya marekebisha yoyote kwenye katiba iliyopitishwa na Mkutano Mkuu.
- 12.11 Baada ya Kamati ya Katiba kumaliza kuandaa katiba iliyopitishwa:
- (a) Mwenyekiti na Katibu Mkuu watatia saina zao kwenye Katiba kuthibitisha kupitishwa kwake kwenye Mkutano Mkuu; na
  - (b) Katiba iliyosainiwa kwenye nakala za kutosha itawasilishwa kwa mamlaka zinazohusika ili isajiliwe.

## SURA YA KUMI NA TATU

### 13 Kuanza kutumika kwa Katiba hii

- 13.1 Katiba hii imepitishwa na wanaumojia kwenye Mkutano Mkuu na kuanza kutumika leo siku ya.....mwezi wa.....2016.

.....  
Jina la Mweka Hazina

.....  
Saini

.....

Jina la Katibu Mkuu

.....

Saini

.....

Jina la Mwenyekiti

.....

Saini